HOTUBA YA WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA, MHE. DKT. ABDALLAH O. KIGODA (MB.), AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA 2015/2016

YALIYOMO

1.0 UTANGULIZI 1
2.0 MIPANGO NA MALENGO YA WIZARA KWA MWAKA 2014/2015 9
3.0 MAFANIKIO YA SEKTA YA VIWANDA NA BIASHARA 2014/2015 13
4.0 SEKTA YA VIWANDA 13
4.1 Uwekezaji na Uzalishaji Unaofanywa na Sekta Binafsi ..14
4.2 Uendelezaji Viwanda vya Kimkakati 20
4.3 Ufufuaji wa Kiwanda cha Matairi cha General Tyre (EA), Arusha 26
4.4 Ufufuaji Kiwanda cha Kilimanjaro Machine Tools, Moshi27
4.5 Ujenzi wa Kiwanda cha Viuadudu –TAMCO (Kibaha) ..28
4.6 Uendelezaji Viwanda vya Nyama.....29
4.7 Kilimo cha Michikichi na Usindikaji Mawese-Mkuranga ..29
4.8 Maeneo Maalumu ya Uwekezaji Chini ya EPZA.....30
4.9 Uendelezaji Viwanda Vidogo na Ujasiriamali 32
4.10 Utafiti katika Uendelezaji Viwanda.....38
4.11 Ujuzi na Weledi katika Uzalishaji Viwandani.....43
4.12 Ujuzi na Weledi katika Biashara.....45
4.13 Sensa ya Viwanda 46
4.14 Programu Mahsusi za Kuongeza Tija na Ufanisi Viwandani 47
4.15 Uendelezaji Viwanda Kikanda 48
5.0 SEKTA YA BIASHARA NA MASOKO 49
5.1 Sekta ya Biashara 49
5.2 Sekta ya Masoko 55
6.0 MAPATO NA MATUMIZI 65
6.1 Mapato 65
6.2 Matumizi 65
7.0 MAENDELEO YA RASILIMALI WATU66

8.0 HUDUMA ZA SHERIA 67
9.0 MAMBO MTAMBUKA..... 67
9.1 Masuala ya Jinsia 67
9.2 Kupambana na Rushwa.....68
9.3 Kupambana na UKIMWI / VVU 69
10.0 MALENGO YA MWAKA 2015/2016 . 69
10.1 Sekta ya Viwanda 69
10.2 Sekta ya Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo.....71
10.3 Sekta ya Biashara.....73
10.4 Sekta ya Masoko 74
11.0 TAASISI CHINI YA WIZARA 76
11.1. Kituo cha Zana za Kilimo na Teknolojia Vijijini (CAMARTEC) 76
11.2 Shirika la Uhandisi na Usanifu wa Mitambo (TEMDO)77
11.3 Taasisi ya Utafiti na Maendeleo ya Viwanda (TIRDO) 78
11.4 Shirika la Viwango Tanzania (TBS) 80
11.5 Baraza la Ushindani (FCT) 81
11.6 Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) 82
11.7 Tume ya Ushindani (FCC).....84
11.8 Baraza la Taifa la Utetezi wa Mlaji (NCAC).....84
11.9 Bodi ya Leseni za Maghala (TWLB).....85
11.10 Chama cha Hakimiliki Tanzania (COSOTA) 87
11.11 Wakala wa Vipimo (WMA).....88
11.12 Shirika la Maendeleo la Taifa (NDC).....89
11.13. Mamlaka ya Maeneo Maalum ya Kuzalisha Bidhaa za Kuuza Nje (EPZA).....91
11.14 Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE) 92
11.15 Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo (SIDO).....93
11.16 Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (TANTRADE) 95
11.17 Kituo cha Biashara cha Tanzania Dubai- (TTC-DUBAI).....97

11.18 Kituo cha Biashara cha Tanzania London (TTC-LONDON) 98
12.0 MASUALA MTAMBUKA..... 99
12.1 Maendeleo ya Rasilimali Watu 99
12.2 Kudhibiti Rushwa 100
12.3 Janga la UKIMWI na Magonjwa Sugu Yasiyoambukizwa 101
12.4 Masuala ya Jinsia 101
13.0 MAOMBI YA FEDHA KWA MWAKA 2015/2016 102
13.1 Mapato ya Serikali 102
13.2 Maombi ya Fedha 102
14.0 HITIMISHO..... 106
VIAMBATISHO 108

ORODHA YA VIFUPISHO

ACT	Agricultural Council of Tanzania
AGOA	African Growth and Opportunity Act
BRELA	Business Activities Registration and Licensing Agency
CAMARTEC	Centre for Agricultural Mechanization and Rural Technology
CBE	College of Business Education
CCM	Chama Cha Mapinduzi
CHC	Consolidated Holdings Corporation
COMESA	Common Market for Eastern and Southern Africa
COSOTA	Copyright Society of Tanzania
COSTECH	Commission for Science and Technology

CTI	Confederation of Tanzania Industries
DANIDA	Danish International Development Agency
DASIP	District Agricultural Sector Investment Project
DFID	Department for International Development
DIT	Dar es Salaam Institute of Technology
EAC	East African Community
EBA	Everything But Arms
EPA	Economic Partnership Agreement
EPZ	Export Processing Zone
EPZA	Export Processing Zone Authority
EU	European Union
FCC	Fair Competition Commission
FCT	Fair Competition Tribunal
GDP	Gross Domestic Product
GTEA	General Tyre East Africa
ICGI	Industrial Credit Guarantee Initiative
IDSL	Industrial Development Support Loan
IFAD	International Fund for Agricultural Development
JBC	Joint Border Committee
JICA	Japan International Cooperation Agency
KCB	Kilimanjaro Cooperative Bank

KNCU	Kilimanjaro Native Cooperative Union
KOICA	Korea International Cooperation Agency
LAT	Leather Association of Tanzania
MOWE	Month of Women Entrepreneurs
MUVI	Muunganisho wa Ujasiriamali Vijijini
MVIWATA	Mtandao wa Vikundi vya Wakulima Tanzania
NDC	National Development Corporation
NEDF	National Entrepreneurship Development Fund
NEMC	National Environment Management Council
NMB	National Microfinance Bank
NMDF	National Marketing Development Forum
NTBs	Non Tariff Barriers
ODOP	One District One Product
OPRAS	Open Performance Review and Appraisal System
OSBP	One Stop Border Post
PPP	Public Private Partnership
RLDC	Rural Livelihood Development Company
SADC	Southern African Development Community
SEZ	Special Economic Zone

Sida	Swedish International Development Agency
SIDO	Small Industries Development Organization
SMEs	Small and Medium Enterprises
TAGMARK	Tanzania Agricultural Marketing Development Trust
TAHA	Tanzania Horticulture Association
TanTrade	Tanzania Trade Development Authority
TBS	Tanzania Bureau of Standards
TCCIA	Tanzania Chamber of Commerce, Industry and Agriculture
TCIMRL	Tanzania China International Mineral Resources Limited
TEMDO	Tanzania Engineering, Manufacturing and Design Organization
TFDA	Tanzania Food and Drug Authority
TIB	Tanzania Investment Bank
TIRDO	Tanzania Industrial Research and Development Organization
TRA	Tanzania Revenue Authority
TTIS	Tanzania Trade Integrated Strategy
TWLB	Tanzania Warehouse Licensing Board
UKIMWI	Upungufu wa Kinga Mwilini
UNCTAD	United Nations Conference on Trade and Development

UNDP	United Nations Development Programme
UNIDO	United Nations Industrial Development Organization
USAID	United States Agency for International Development
WMA	Weights and Measures Agency
WTO	World Trade Organization

HOTUBA YA WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA, MHE. DKT. ABDALLAH O. KIGODA (MB.), AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA 2015/2016

1.0 UTANGULIZI

1. ***Mheshimiwa Spika,*** kutokana na taarifa iliyowasilishwa leo hapa Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uchumi, Viwanda na Biashara, ambayo ilichambua Bajeti ya Wizara ya Viwanda na Biashara tarehe 5 - 6 Mei, 2015, Jijini Dar es Salaam, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu sasa likubali kupokea, kujadili na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha ya Wizara ya Viwanda na Biashara kwa mwaka 2015/2016.

2. ***Mheshimiwa Spika,*** naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kwa baraka zake na kutukirimu afya njema leo na hivyo kutuwezesha kumudu kutekeleza majukumu ya Taifa letu kwa mwaka 2014/2015, na kwa jumla katika kipindi chote cha miaka 10 ya Awamu ya Nne ya uongozi wa Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

3. ***Mheshimiwa Spika,*** nathubutu kutamka kwamba katika kipindi hiki cha Serikali ya Awamu ya Nne, mafanikio makubwa yamepatikana katika Sekta ya Viwanda na Biashara. Aidha, kama nitakavyoeleza katika Hotuba yangu, Serikali ya Awamu ya Nne imeweka pia msingi imara wa maendeleo endelevu ya Sekta ya Viwanda na Biashara na Taifa letu kwa jumla.

4. ***Mheshimiwa Spika,*** hivyo sina budi kumshukuru kwa namna ya kipekee kabisa Mheshimiwa Rais kwa imani yake kubwa kwangu kwa kunikabidhi dhamana hii kubwa, muhimu na nyeti Kitaifa. Ni dhamana nyeti kwa sababu Sekta ya Viwanda na Biashara ndiyo Sekta Kiongozi katika kuleta mageuzi ya kiuchumi na kijamii katika Taifa lolote lile Duniani lililodhamiria kupiga maendeleo ya haraka ya kiuchumi na kijamii. Nina hakika kuwa nimetumia juhudi na uwezo wangu wote kutekeleza kazi na dhamana hii niliyopewa na Mheshimiwa Rais. Ni matumaini yangu kuwa mafanikio tuliyofikia yataendelezwa kwa nguvu na msukumo wa ziada katika uongozi wa Serikali ya Awamu ya Tano katika Taifa letu.

5. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mantiki hiyo naomba kutumia fursa hii na kwa namna ya kipekee kabisa kumpongezi Mheshimiwa Dkt.

Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kusimamia kwa umakini mkubwa mipango ya Kitaifa na Kimataifa, hususan uendelezaji wa Sekta ya Viwanda na Biashara; Uchumi; Mchakato wa Uuandaaji Katiba Mpya ya Taifa letu; na Chaguzi za Serikali za Mitaa ambazo zinatuelekeza katika Uchaguzi Mkuu wa Taifa hapo mwezi Oktoba, 2015.

6. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi hiki kilichobakia napenda kumhakikishia Mheshimiwa Rais kuwa, kazi ya kuendeleza Sekta hii tutaifikisha mahala penye mwelekeo mzuri katika kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya mwaka 2010 na malengo ya Dira ya Taifa ya Maendeleo ya 2025.

7. ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, napenda kuipongeza Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uchumi, Viwanda na Biashara, chini ya uenyekiti wa Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina, Mbunge wa Kisesa (CCM), na Makamu wake, Mheshimiwa Dunstan Luka Kitandula, Mbunge wa Mkinga (CCM), na Waheshimiwa Wajumbe wote wa Kamati hiyo. Ushauri na maelekezo ya Kamati na Waheshimiwa Wabunge wa Bunge lako Tukufu kwa jumla tuna uthamini na kuuzingatia katika kuandaa na kuboresha Hotuba ninayoiwasilisha. Kwa msingi huo,

napenda kutumia fursa hii kuwaombea kwa Mungu na Wapiga Kura wao ili sote turudi katika Bunge lijalo kuendeleza na kukamilisha malengo yetu tuliyojiwekea katika Sekta ya Viwanda na Biashara.

8. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa namna ya kipekee napenda kukushukuru wewe binafsi, Mheshimiwa Spika, Naibu Spika, Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Bunge, Katibu wa Bunge na Watendaji wote wa Ofisi ya Bunge la Tanzania kwa ushirikiano mzuri ambao Wizara na Wadau wetu wameendelea kuupata toka kwenu. Ni dhamira yetu kuuendeleza na kuudumisha ushirikiano huo katika Awamu zijazo za Uongozi wa Taifa letu ili kuleta mapinduzi ya viwanda kama ilivyobainishwa katika Dira 2025.

9. ***Mheshimiwa Spika***, aidha, namshukuru na kumpongeza sana Mhe. Mizengo Peter Pinda, maarufu kama *Mtoto wa Mkulima*, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mbunge wa Jimbo la Katavi (CCM), kwa Hotuba yake iliyobeba busara na maelekezo stahiki, yenye dira na mwelekeo sahihi katika kukamilisha Utekelezaji wa Mipango na Programu za Serikali ya Awamu ya Nne kwa mwaka 2015/2016. ***Mheshimiwa Spika***, pamoja na kuwepo changamoto kadhaa

za Kitaifa na Kimataifa bado Mheshimiwa Pinda ametoa mchango mkubwa sana katika kuendeleza viwanda nchini na hususan katika utafutaji wa rasilimali za utekelezaji wa Miradi ya Kimkakati ya Sekta ya Viwanda na Biashara. Si hivyo tu, lakini hatua yake ya kuvalia njuga dhana ya **KILIMO KWANZA** imesaidia katika kukuza Sekta ya Viwanda na Biashara. Aidha, nawapongeza Mawaziri walionitangulia kuwasilisha hoja zao hapa Bungeni.

10. ***Mheshimiwa Spika,*** nichukue fursa hii pia kumpongeza, Mhe. George Mcheche Masaju, kwa kuteuliwa kuwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Pia, nawapongeza Waheshimiwa Dkt. Grace K. Puja (Mb) na Innocent R. Sebba (Mb) kwa kuteuliwa kuwa Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, nawapongeza pia walioteuliwa na Mhe. Rais kuwa Mawaziri na Naibu Mawaziri kuongoza Wizara mbalimbali hadi sasa. Uteuzi wao unaonesha ni jinsi gani Mheshimiwa Rais ana imani nao katika kuendeleza Taifa letu na wananchi kwa jumla.

11. ***Mheshimiwa Spika,*** napenda kutumia fursa hii kuwashukuru kwa dhati kabisa wapiga kura wangu wote wa Jimbo la Handeni kwa imani yao kwangu; kwa kunitia moyo na kunipa ushirikiano mzuri ulioniwezesha kutekeleza

majukumu yangu kama Waziri na pia Mwakilishi wao katika Bunge hili Tukufu. Naishukuru pia familia yangu hususan mke wangu, watoto, ndugu na jamaa kwa dua zao na ushirikiano wao mzuri ulioniwezesha kuwatumikia Watanzania na hususan Wanaviwanda na Wafanyabishara bila ya kuchoka. Nawaombeni kuwa tuendelee kushirikiana sasa na siku zijazo. Siku zote nasisistiza kuwa mambo mazuri hayataki haraka bali yanahitaji umakini na dhamira yakufikia malengo yaliyowekwa.

12. ***Mheshimiwa Spika*****,** vilevile, naomba kutumia fursa hii kuwashukuru Viongozi na Watendaji wote wa Wizara, Taasisi za Serikali na wadau wote. Kwa uchache, napenda kuwatambua wafuatao: Baraza la Taifa la Biashara - TNBC; Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania - TPSF; Shirikisho la Wenye Viwanda Tanzania - CTI; Chama cha Wafanyabiashara, Viwanda na Kilimo Tanzania - TCCIA; Baraza la Kilimo Tanzania - ACT; Chama cha Wadau wa Ngozi Tanzania - LAT; Chama cha Wafanyabiashara Wanawake - TWCC; na Vikundi vya Biashara Ndogo (VIBINDO) kwa michango yao katika kuendeleza Sekta ya Viwanda na Biashara. Nawashukuru pia wananchi wote, waandishi na wamiliki wa vyombo vya habari kwa mchango wao mkubwa

katika kuelimisha umma wa Watanzania kuhusiana na utendaji wa Wizara na uendelezaji wa Sekta ya Viwanda, Biashara, na Masoko; kuvutia wawekezaji na kuhimiza uzalishaji viwandani. Ni matumaini yangu kuwa, ari na ushirikiano huo utaendelezwa siku zijazo.

13. ***Mheshimiwa Spika,*** Hotuba hii ni matokeo ya uratibu na ushirikiano mzuri wa Viongozi wenzangu katika Wizara, akiwemo Naibu Waziri, Mhe. Janet Z. Mbene (Mb.); Katibu Mkuu, Bw. Uledi A. Mussa, Naibu Katibu Mkuu, Bibi. Maria H. Bilia; Wakuu wa Idara, Vitengo, Taasisi na watumishi wote wa Wizara. Nawapongeza kwa kuongoza na kusimamia utekelezaji wa majukumu ya kisekta. Namshukuru pia Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali na wachapishaji wengine kwa kuchapisha machapisho mbalimbali ya Wizara yangu kwa wakati.

14. ***Mheshimiwa Spika,*** nawashukuru pia Wadau wetu wa Maendeleo, zikiwemo nchi rafiki ambazo ni pamoja na Austria, Canada, China, Denmark, Finland, India, Ireland, Japan, Korea ya Kusini, Marekani, Norway, Sweden, Uholanzi, Uingereza, Ujerumani na Uswisi. Aidha, Mashirika ya Kimataifa ni pamoja na: ARIPO, Benki ya Dunia, CFC, DANIDA, DFID, EU, FAO,

IFAD, JICA, Jumuiya ya Madola, KOICA, Sida, UNCTAD, UNDP, UNIDO, USAID, WIPO na WTO.

15. ***Mheshimiwa Spika,*** naomba kuwapa pole ndugu na jamaa kwa kuondokewa na mpendwa wetu, Mhe. Kapt. John Damiano Komba, aliyekuwa Mbunge wa Mbinga Magharibi (CCM). Vilevile, nawapa pole wananchi waliokumbwa na kadhia ya mafuriko yaliyotokea nchini mwaka huu na kusababisha vifo, majeruhi na uharibifu mkubwa wa mali. Mwenyezi Mungu awarehemu wale wote waliotutoka na pia kuwapa ahueni haraka waliojeruhiwa katika kadhia hii.

16. ***Mheshimiwa Spika,*** kama tunavyofahamu, mwaka 2015 ni mwaka wa Uchaguzi Mkuu kwa Taifa letu ambapo tutachagua uongozi wa Kitaifa wa Serikali ya Awamu ya Tano. Hivyo, napenda kuungana na viongozi wenzangu kuwatakia kila la kheri Watanzania wote katika Uchaguzi Mkuu ujao na naomba kutumia fursa hii kuwaomba Watanzania wenye sifa za kupiga kura wajiandikishe na kupiga kura ili watumie haki yao ya kikatiba. **Mheshimiwa Spika,** natumai kuwa wananchi watajitokeza kwa wingi kujiandikisha na kisha kupiga kura ili kupata uongozi makini utakaoendeleza uzalendo,

amani, mshikamano, utulivu na kulinda mafanikio tuliyopata.

2.0 MIPANGO NA MALENGO YA WIZARA KWA MWAKA 2014/2015

17. ***Mheshimiwa Spika,*** utekelezaji wa majukumu ya Wizara yetu kwa mwaka 2014/2015 ulizingatia Mpango Mkakati wa Wizara wa miaka mitano, yaani 2011/2012 – 2015/2016 na Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025. Aidha, Wizara imekuwa ikitekeleza Malengo ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2010; na Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini (MKUKUTA II). Kwa kuzingatia miongozo hiyo ya kisera na kimkakati, Wizara ya Viwanda na Biashara, katika kipindi cha mwaka 2014/2015, iliweka msukumo mkubwa katika kuimarisha uzalishaji na tija katika viwanda vilivyopo; kuhimiza ujenzi wa viwanda vipya ili kuongeza uwezo wa uzalishaji na michepuo ya bidhaa; kuhimiza mauzo ya bidhaa na huduma nje ya nchi; kushirikiana na Sekta Binafsi katika uanzishaji na uendelezaji viwanda vya msingi na vya kimkakati kupitia taasisi zake za NDC na EPZA; kuendeleza na kuimarisha taasisi za utafiti na maendeleo ya viwanda; uboreshaji wa mazingira ya ufanyaji biashara na uzalishaji; na kuendeleza taaluma na weledi wa

watumishi wake ili kutoa huduma bora zaidi kwa wadau. Madhumuni ya hatua zote hizo ilikuwa ni kuchangia katika uboreshaji wa uchumi wa Taifa ili kujenga Taifa linalojitegemea na linaloongozwa na uchumi wa viwanda ifikapo mwaka 2025. Katika Aya zifuatazo za Hotuba yangu hii naelezea kwa kina mafanikio ya utekelezaji wa hatua hizo.

18. ***Mheshimiwa Spika,*** kabla ya kuelezea kwa kina mafanikio yaliyopatikana katika Sekta ya Viwanda na Biashara kwa mwaka 2014/2015, niruhusu nirejee dhana niliyoigusia katika Hotuba yangu iliyopita. Katika Hotuba hiyo, nilibainisha kuwa dhana mpya inayotamalaki hivi sasa katika medani ya Ushirikiano wa Kikanda na Kimataifa ni ifuatayo:

Uchumi ni Siasa badala ya dhana ya zamani ya ***Siasa ni Uchumi.***

19. ***Mheshimiwa Spika,*** athari za dhana hiyo mpya ni kwamba Mataifa yenye uchumi duni na usiogusa kila tabaka la jamii katika nchi yataendelea kuyumba kisiasa. Mathalan, Vuguvugu la Nchi za Kiarabu, maarufu kama *Arab Spring*, chimbuko lake ni uchumi na si kukosekana kwa demokrasia. Hivyo, uchumi unaogusa kila mtu katika Taifa, kuanzia wale

wenye vipato vya chini, vya kati na vya juu, vijijini na mijini, msingi wake lazima ujengwe juu ya viwanda na biashara. Ndiyo, maana Serikali ya Awamu ya Nne imeweka mkazo mkubwa katika uendelezaji Viwanda na Biashara.

20. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Awamu hii ya Nne, mikakati ya uendelezaji viwanda imeboreshwa kwa kurejea nafasi ya Dola katika uanzishaji na uendelezaji viwanda vya msingi na vya kimkakati. Nafasi ya Serikali hivi sasa inajitokeza katika uwekezaji wa moja kwa moja katika uendelezaji viwanda na utekelezaji wa program mbalimbali kwa ushirikiano kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi, kama njia mojawapo ya kuharakisha maendeleo ya kiuchumi na kiteknolojia. ***Mheshimiwa Spika,*** bila kutumia mikakati ya aina hiyo ni dhahiri kuwa uendelezaji wa miradi mikubwa kama Miradi ya Makaa ya Mawe Mchuchuma na Chuma Liganga ingekuwa ndoto tu hadi sasa.

21. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mfano, mchakato wa uendelezaji wa miradi ya Makaa ya Mawe Mchuchuma na Chuma Liganga ulianza miaka ya 1950 walipoendesha utafiti wa kwanza mkubwa mwaka 1958 bila mafanikio na hadithi imekuwa hiyohiyo hadi tulipofanikiwa katika Serikali ya Awamu ya Nne baada ya kuamua

kutumbukiza mkono wake na dhamana hiyo kukabidhiwa katika Wizara yangu. Sasa utafiti na usanifu wa kina umekamilishwa chini ya miaka miwili tu na pia Mwekezaji Mwenza wa Kimkakati na fedha za utekelezaji takriban shilingi trilioni 5.0 kupatikana. Jambo linalosubiriwa sasa ni uletaji wa mitambo na vifaa vingine vya ujenzi ili Mheshimiwa Rais aweze kuzindua kabla ya kumaliza kipindi chake cha Uongozi. Huo utakuwa uwekezaji mkubwa katika mradi mmoja wa viwanda tangu Tanzania ipate uhuru wake mwaka 1961.

22. ***Mheshimiwa Spika,*** ushiriki wa Sekta ya Umma, yaani Dola, katika uendelezaji viwanda na miradi mbalimbali ya kimkakati katika uchumi unaonekana katika miradi mingine mikubwa inayotekelezwa na NDC na EPZA. Mathalan, ujenzi wa Kiwanda cha Viuadudu Kibaha kwa ajili ya kudhibiti Malaria; Mradi wa Magadi huko Engaruka; na Umeme wa Upepo katika Mkoa wa Singida na Makambako, Mkoa wa Njombe; uendelezaji Maeneo Maalum ya Uwekezaji katika Mikoa ya Dar es Salaam, Pwani, Tanga, Mtwara na Kigoma. Hayo ni maeneo ya mwanzo tu na hivyo siku hadi siku maeneo mengine yatabainishwa. Hadi mwishoni mwa mwaka 2014, kiasi cha uwekezaji katika maeneo Maalum ya Uwekezaji ulifikia Dola za

Marekani bilioni 1.3, sawa na Shilingi Trilioni 2.4 na ajira 32,000.

3.0 MAFANIKIO YA SEKTA YA VIWANDA NA BIASHARA 2014/2015

4.0 SEKTA YA VIWANDA

23. ***Mheshimiwa Spika,*** napenda nilitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa Tanzania imekuwa chaguo namba moja kwa wawekezaji katika Kanda hii (*Tanzania is the preferred destinations for industrial investment in the region).* Mathalan, hadi Robo ya Pili ya mwaka 2014/2015, jumla ya miradi ya viwanda vipya iliyosajiriwa ni 124, sawa na wastani wa viwanda 20 kwa mwezi. Hali hiyo imefanya kuwepo uhaba mkubwa wa maeneo yanayofaa kwa uwekezaji viwanda nchini kiasi cha Wizara kuwaomba Viongozi wa Mikoa na Halmashauri kutenga maeneo mahsusi kwa kazi hiyo. ***Mheshimiwa Spika,*** hivyo, naomba kutumia fursa hii kuishukuru Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa mchango wake mkubwa katika kuchukua hatua ya kuhakikisha kuwa kutoka sasa Mipango Miji yote inazingatia utengaji wa maeneo ya uendelezaji viwanda na ufanyaji biashara. Vivyo hivyo, napenda kutambua mwitikio wa Wakuu wa Mikoa na Wilaya katika mchakato huu.

24. ***Mheshimiwa Spika,*** ukiacha maeneo ya EPZ/SEZ, Wizara pia imeanza kutafuta maeneo ya uwekezaji katika maeneo mbalimbali nchini. Kwa mfano mwaka 2014/2015, Wizara imepata eneo la ekari 107 kutoka Mamlaka ya Ustawishaji Makao Makuu, Dodoma kwa lengo la kuanzisha Mitaa ya Viwanda *(Industrial Parks).* Tayari kazi za kupima, kuweka mipaka na kuandaa michoro/ramani ya eneo husika imefanyika na hatimiliki kupatikana. Vilevile, Manispaa ya Singida imetenga eneo lenye ukubwa wa ekari 120 katika Kata ya Ng'aida kwa ajili hiyo hiyo. ***Mheshimiwa Spika,*** baada ya maelezo hayo mafupi ya utangulizi sasa naomba nieleze kwa kina utekelezaji katika Sekta ya Viwanda kwa mwaka 2014/2015.

4.1 Uwekezaji na Uzalishaji Unaofanywa na Sekta Binafsi

4.1.1 Viwanda vya Kemikali

25. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Sekta Ndogo ya Viwanda vya Kemikali, kumekuwepo mafanikio makubwa. Kwa mfano, ujenzi wa viwanda vitatu vikubwa vya Saruji huko Mkoani Mtwara, Tanga na Pwani utaliwezesha Taifa kujitosheleza kwa Saruji na kuwa na ziada ya

kuuzwa nje. Msingi wa hoja hiyo ni kwamba kati ya viwanda hivyo vitatu vipya kimojawapo kina uwezo wa kuzalisha kiasi cha saruji sawa na uzalishaji wa viwanda vyote vya saruji vilivyopo nchini hivi sasa. Miradi ambayo imekamilika katika kipindi hiki na uzalishaji kuanza kwa kutumia *clinker* kutoka nje ya nchi ni viwanda vya *Lee Building Materials Company Limited* kilichopo Kilwa Masoko (Lindi) na *Rhino Cement Company* kilichopo Mkuranga (Pwani). Kuanzishwa kwa viwanda hivyo, kumewezesha uzalishaji wa saruji kuongezeka kutoka tani milioni 3.06 mwaka 2013 hadi tani milioni 4.4 mwaka 2014, sawa na ongezeko la asilimia 11.11. Hii inatokana na kuanza kufanya kazi kwa viwanda vipya vinne (4) vya *Rhino Cement Co. Ltd, Lee Building Materials Ltd, Camel Cement Co. Ltd* na *Lake Cement Company Ltd.* Aidha, kuna miradi takriban minane (8) ya Viwanda vya Saruji ambayo iko katika hatua mbalimbali za ujenzi ambayo ni pamoja na *Arusha Cement Co. Ltd, Kisarawe Cement Co. Ltd, Sungura Cement Ltd, Fortune Cement Co. Ltd, MEIS Industries Ltd, Maweni Limestone Co. Ltd* na *Dangote Cement Co. Ltd*.

26. ***Mheshimiwa Spika***, hivyo ni dhahiri basi kuwa azma ya Serikali ya Awamu ya Nne ya kuhakikisha bei ya saruji nchini inashuka itafikiwa na hivyo kupunguza gharama za ujenzi

ili kuwawezesha Watanzania walio wengi kupata makazi yenye hadhi na salama. Wizara itaendelea kuboresha mazingira ya uwekezaji wa viwanda vya saruji ili kufikia malengo tuliojiwekea kama Taifa.

4.1.2 Viwanda vya Nguo na Mavazi

27. ***Mheshimiwa Spika,*** Sekta ya Nguo na Mavazi, kihistoria na kwa asili yake ni sekta yenye uwezo wa kuzalisha ajira nyingi na pia kuinua maisha ya wazalishaji pamba. Kutokana na umuhimu huo, Wizara imeunda Kitengo mahsusi cha kusimamia maendeleo ya Sekta Ndogo ya Nguo na Mavazi. Kupitia Kitengo hicho, Wizara imeendelea kutekeleza Mkakati wa Kuendeleza Sekta ya Nguo na Mavazi ambao umewezesha viwanda kadhaa vipya kuanzishwa ikiwemo kiwanda kipya cha usokotaji nyuzi cha DAHONG kilichopo Mkoani Shinyanga. Kiwanda hicho kina uwezo wa kutumia pamba yote izalishwayo katika Kanda ya Ziwa, na kinategemea kuanza uzalishaji mapema zaidi ikilinganishwa na muda uliotarajiwa awali. Hatua hiyo, itatatua changamoto ya soko la pamba lisilo la uhakika na bei isiyoridhisha kwa wakulima wetu wa Kanda ya Ziwa. Aidha, Kiwanda cha Mavazi cha TOOKU kilichopo Dar es Salaam kimeanzishwa kupitia Mkakati wa

EPZ na kina uwezo wa kuajiri watu 14,000 na kimeanza uzalishaji.

28. ***Mheshimiwa Spika,*** somo tulilojifunza litokanalo na uwekezaji huo ni kwamba Kitaifa tuna uhaba mkubwa wa Kada ya Washonaji Mahiri wa Mavazi. Kwa mfano, Kiwanda cha TOOKU kimeweza kuwaajiri wafanyakazi 3,000 tu, kati ya 14,000 kinaowahitaji. Hali hiyo imeilazimu Wizara, katika mwaka 2014/2015, kuchukua hatua za kukiunganisha Kiwanda hicho na kituo mahiri cha mafunzo ya washonaji mavazi cha GOIG kilichopo Jijini Dar es Salaam na pia kuishauri VETA kuangalia upya mfumo wake wa mafunzo ili uendane na mahitaji ya Sekta ya Viwanda. Kituo cha GOIG kinapata msaada wa wakufunzi wa ushonaji na ufundi wa vifaa vya ushonaji kutoka Serikali ya Finland na hivyo kimebobea katika fani hiyo, jambo ambalo VETA wanaweza kujifunza katika uendeshaji wa mafunzo yao.

4.1.3 Sekta Ndogo ya Ngozi

29. ***Mheshimiwa Spika,*** eneo jingine ambalo Wizara imeendelea kuweka mkazo katika mwaka 2014/2015 ni usindikaji ngozi. Wizara imebaini kuwa ufugaji, na hususan wa ng'ombe, mbuzi na kondoo una tija ndogo kwa wafugaji wetu nchini. Chimbuko la hali hiyo ni

matumizi ya teknolojia isiyofaa katika usindikaji nyama. Katika mataifa yaliyopiga hatua kubwa ya maendeleo katika matumizi ya bidhaa za mifugo utakuta takriban asilimia 95 ya mnyama ina manufaa fulani, yaani ni sehemu ndogo sana inayotupwa. Kwa mfano nchini India katika Kiwanda cha Nyama cha Allana Group, mnyama akichinjwa, hutoa nyama, mifupa yake husagwa na kuwa malighafi ya kutengenezea dawa ya meno, damu hutumika kuzalisha chakula cha mifugo na ngozi husindikwa kutengeneza bidhaa za ngozi.

30. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara yangu kwa kushirikiana na Wizara ya Mifugo na Maendeleo ya Uvuvi na wadau wengine, katika mwaka 2014/2015, ilianza kuifanyia kazi dhana ya matumizi kamilifu ya mnyama aliyechinjwa, kwanza kwa kuwashawishi wawekezaji mahiri katika eneo hili na pia kuhimiza usindikaji ngozi nchini badala ya uuzwaji wa ngozi ghafi. Wizara inaendelea kufuatilia wawekezaji ambao wameonyesha nia ya kuwekeza katika kiwanda cha kisasa cha nyama na pia kuwasaidia NARCO kiufundi na kiteknolojia katika mchakato wao wa kuanzisha Kiwanda cha Nyama huko Kibaha. Aidha, Wizara imedhamiria kuufanya uuzaji ngozi ghafi nje ya nchi kuwa historia. Tayari, ujenzi wa viwanda vikubwa viwili, Arusha (*Meru Tannery*) na Shinyanga

(*Xing Hua Investment Ltd.)* umekalimika ambavyo kwa pamoja vitaweza kusindika ngozi yote ghafi inayozalishwa katika Kanda ya Kaskazini na Kanda ya Ziwa. Pamoja na kukabiliana na changamoto ya magendo ya ngozi ghafi, uwekezaji huo utasaidia katika kuongeza kipato cha wafugaji ambao kwa kipindi kirefu wamekuwa hawafaidiki na ngozi, ziwe za ng'ombe, mbuzi au kondoo. Hatua hiyo imeongeza usindikaji ngozi za ng'ombe kutoka vipande vya ngozi 1,060,777 mwaka 2013/2014 hadi vipande 1,388,139 mwaka 2014/2015, sawa na ongezeko la asilimia 31. Ongezeko hilo limetokana na uwekezaji katika viwanda vipya vya ngozi vya Arusha na Shinyanga. Aidha, ujenzi wa Kiwanda cha *Gobosh* chenye uwezo wa kusindika tani 500,000 Mkoani Mwanza unaendelea na Kiwanda cha *Huacheng* Mkoani Dodoma chenye uwezo wa kusindika futi za mraba milioni 20 za ngozi kwa mwaka kwa sasa kinafanyiwa majaribio ya uzalishaji baada ya ujenzi kukamilika.

31. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kujenga uwezo wa kiufundi na ujuzi, katika mwaka 2014/2015, Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia imewezesha Chuo cha Teknolojia Dar es Salaam – Kampasi ya Mwanza kuanza kutoa mafunzo ya Stashahada ya Taaluma ya Ngozi (Ordinary

Diploma in Leather Technology); mafunzo ya teknolojia ya utengenezaji viatu kwa njia ya mtandao kwa washiriki 88 kutoka mikoa 9 ya Tanzania Bara. Washiriki katika mafunzo hayo walitoka katika mikoa ya Arusha, Dar es salaam, Kilimanjaro, Lindi, Manyara, Mtwara, Mwanza, Pwani na Singida. Aidha, Zanzibar pia ilishirikishwa katika mafunzo hayo.

4.2 Uendelezaji Viwanda vya Kimkakati

32. ***Mheshimwa Spika,*** siri kubwa ya maendeleo ya haraka kiviwanda ambayo Jamhuri ya Watu wa China imeweza kuyapata katika Karne hii ni ushiriki wa moja kwa moja wa Dola katika kuanzisha na kuendeleza miradi ya Viwanda vya Msingi na Programu za Kimkakati katika uchumi. Hivyo, Serikali ya Awamu ya Nne na Chama Tawala imeendelea kutekeleza dhana hiyo ya ushiriki wa Serikali katika uchumi badala ya kuiachia Sekta Binafsi pekee. Ushiriki wa Serikali katika uwekezaji unafanywa kupitia taasisi zake za NDC, EPZA na SIDO.

33. ***Mheshimwa Spika,*** katika juhudi za kuendeleza Viwanda Mama na vya Kimkakati Nchini, Wizara kupitia NDC imeendelea kutekeleza miradi ya kuzalisha umeme kwa kutumia makaa ya mawe ya Mchuchuma na

Ngaka Kusini; Chuma huko Liganga na Maganga Matitu; Umeme kutokana na nguvu ya upepo huko Singida; Viuadudu vya kuua Viluwiluwi vya mbu waenezao Malaria huko Kibaha, Pwani; Magadi Soda Engaruka, Monduli - Arusha; Ufufuaji wa Kiwanda cha Kutengeneza Matairi cha *General Tyre (EA) Ltd*, Arusha; Kiwanda cha Kutengeneza Vipuri na Mashine cha *Kilimanjaro Machine Tools Co. Ltd (KMTC)*, Kilimanjaro; Uendelezaji Mashamba ya Mpira ya Kalunga, Morogoro na Kihuhwi, Tanga; Mradi wa Kilimo cha Michikichi na Kiwanda cha Kuzalisha Mafuta ya Mawese, Kisarawe - Pwani; Ujenzi wa Maeneo ya Viwanda (*Industrial Park*s) Kibaha - Pwani, KMTC - Kilimanjaro, Kange - Tanga; na kujenga uwezo wa wananchi wa maeneo ambayo miradi ya kimkakati inatekelezwa ili wafaidike na miradi hiyo.

34. ***Mheshimwa Spika,*** naomba sasa nielezee matokeo ya utekelezaji wa dhana hiyo kwa muhtasari kwa mwaka 2014/2015 kama ifuatavyo:-

4.2.1 Miradi ya Chuma Liganga na Makaa ya Mawe Mchuchuma

35. ***Mheshimiwa Spika,*** Miradi ya Chuma Liganga na Makaa ya Mawe Mchuchuma inatekelezwa na Kampuni ya *Tanzania China International Mineral Resources Limited*

(TCIMRL), ambayo ni Kampuni ya Ubia kati ya NDC na *Sichuan Hongda Group* ya Jamhuri ya Watu wa China. Mradi huo unahusu ujenzi wa kiwanda cha chuma kitakachozalisha tani milioni moja kwa mwaka; kufunga mitambo ya kufua umeme ya megawati 600, ambapo kati ya hizo megawati 250 zitatumika katika kiwanda cha chuma na megawati 350 zitaingizwa katika Gridi ya Taifa. Kiasi hicho cha uzalishaji wa chuma kitaifanya Tanzania kuwa nchi ya tatu Barani Afrika kwa uzalishaji wa chuma. Miradi hiyo itatoa ajira zipatazo 32,000 na mapato ya takribani Dola za Marekani bilioni 1.736 kwa mwaka, sawa na shilingi Trilioni 3.13.

36. ***Mheshimiwa Spika,*** azma ya Wizara katika utekelezaji wa miradi hiyo ya kihistoria ni kwamba Jiwe la Msingi liwekwe na Mheshimiwa Rais, Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, kabla ya kumaliza kipindi chake cha uongozi wa Taifa letu. Hivyo, napenda kutumia fursa hii kuwaomba viongozi na wananchi wa Mkoa wa Njombe kuendelea kutoa ushirikiano wa hali na mali ili kufanikisha utekelezaji wa mradi huo muhimu Kitaifa.

4.2.2 Mradi wa Makaa ya Mawe Ngaka Kusini – Ruvuma

37. ***Mheshimiwa Spika,*** Mradi wa Makaa ya Mawe ya Ngaka Kusini, katika Wilaya ya Mbinga, unatekelezwa na Kampuni ya *TANCOAL Energy Limited*, ambayo ni Kampuni ya ubia kati ya NDC na *Intra-Energy Corporation* ya Australia. Uzalishaji wa makaa ya mawe unaendelea, ambapo kwa kipindi cha kuanzia Januari, 2014 mpaka Machi, 2015 Kampuni ilizalisha tani 327,141 za makaa ya mawe zenye thamani ya takriban shilingi bilioni 25.2. Makaa yam awe hayo huuza katika viwanda vya *Tanga Cement, Mbeya Cement, Lake Cement, Tanzania Gypsum Limited, Mufindi Paper Mills, Simba Lime,* na nyingine huuzwa nchini Kenya, Malawi, Rwanda, Uganda na Zambia. Hivyo, mradi huu una faida kuu nne kwa Taifa letu: unaliingizia Taifa fedha za kigeni; kuokoa matumizi ya fedha za kigeni katika kuagiza mafuta ambayo yangetumika kama nishati katika viwanda husika; kutoa ajira; na kukuza teknolojia. Kwa mantiki hiyo, katika mwaka 2014/2015, Serikali iliendelea kuboresha miundombinu ya barabara na bandari za Ndumbwi na Itungi ili kupunguza gharama za usafirishaji ili makaa ya mawe ya kiwanda hicho yaweze kushindana kwa bei kitaifa na kimataifa. Aidha, TANCOAL inaendelea na mpango wa kujenga kituo cha kufua umeme cha megawati 400 kitakachojengwa Ngaka, Wilaya ya Mbinga kwa kuanzia na megawati 200. Mpango huu

utaanza kutekelezwa mara tu ujenzi wa msongo wa umeme kutoka Makambako mpaka Songea wa kilovoti 220, utakapoanza kujengwa ili kuunganisha na Gridi ya Taifa.

4.2.3 Mradi wa Kuzalisha Chuma Ghafi-Maganga Matitu na Katewaka

38. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi wa kuzalisha Chuma Ghafi-Maganga Matitu na Katewaka unatekelezwa na Kampuni ya *Maganga Matitu Resource Development Limited* (MMRDL), ambayo ni Kampuni ya ubia kati ya NDC na Sekta Binafsi kupitia Kampuni ya *MM Steel Resources Public Limited Company* (MMSR PLC) ambayo ni ya wazawa. Faida mojawapo ya mradi huo ni kwamba utajenga uwezo wa kitaalam kwa Watanzania katika eneo hilo jipya la uzalishaji wa chuma ghafi na Taifa kupata *carbon credit* kutokana na teknolojia hiyo kutokuwa na madhara makubwa kwa mazingira. Uwekezaji umekadiriwa kuwa Dola za Marekani milioni 350. Mradi huo utaingiza kipato cha Dola za Marekani milioni 150 kwa mwaka na kutoa fursa za ajira zipatazo 1,989. Ujenzi wa mradi huo unatarajiwa kuanza katika kipindi cha mwaka 2015/2016.

4.2.4 Mradi wa Umeme wa Upepo-Singida

39. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi wa Umeme wa Upepo-Singida unatekelezwa na Kampuni ya *Geo-Wind Tanzania Limited*, ambayo ni Kampuni ya ubia kati ya NDC, TANESCO na Sekta Binafsi kupitia Kampuni iitwayo *Power Pool East Africa Limited* (PPEAL) ambayo ni ya wazawa. Mradi huo ni moja ya miradi iliyopo katika Mpango wa Matokeo Makubwa Sasa (BRN) na unahusisha usimikaji wa mitambo ya kuzalisha umeme wa megawati 50 kwa kuanzia na baadaye kuongeza mpaka kufikia megawati 300. Uwekezaji kwa megawati 50 pamoja na miundombinu yake inayohusisha *substation* na *transmission line* ni Dola za Marekani milioni 136 ambazo Benki ya EXIM China imekubali kuzitoa kwa masharti nafuu baada ya majadiliano kukamilishwa mwaka 2014/2015. Suala linalosubiriwa sasa ni uwekaji saini wa Mkataba wa Mkopo *(Loan Agreement)* kati ya Wizara ya Fedha na Benki ya EXIM ili ujenzi uanze.

4.2.5 Mradi wa Kuzalisha Magadi Soda – Arusha

40. ***Mheshimiwa Spika,*** Mradi wa Magadi Soda huko Engaruka unaoendelezwa na NDC, unatarajiwa kuzalisha tani milioni moja za magadi na bidhaa nyingine za chumvi kwa mwaka. Ujenzi wa kiwanda cha magadi huko Engaruka utaifanya Tanzania kuwa miongoni

mwa nchi zinazozalisha kwa wingi magadi hayo duniani ikizidiwa na Marekani pekee. Katika kipindi cha mwaka 2014/2015, Wizara, kupitia NDC, ilikamilisha uainishaji wa eneo la kilomita za mraba 410 katika Bonde la Engaruka, Wilayani Monduli linalohitajika katika ujenzi wa kiwanda na miundombinu yake, makazi ya wafanyakazi na viwanda vingine vya kuongeza thamani vinavyotumia magadi soda kama malighafi. Hivi sasa, Wizara kupitia NDC iko katika hatua za mwisho za kumpata mbia atakayeshirikiana na NDC katika kujenga kiwanda hicho.

4.3 Ufufuaji wa Kiwanda cha Matairi cha General Tyre (EA), Arusha

41. ***Mheshimiwa Spika,*** napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kwamba katika mwaka 2014/2015, Wizara, ikishirikiana na wadau mbalimbali ikiwemo Wizara ya Fedha, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Msajili wa Hazina, Ubalozi wetu nchini Ujerumani na NDC, imeweza kufikia makubaliano na Mbia Mwenza katika Kiwanda cha Matairi cha *General Tyre (GTEA)* kilichopo Arusha. Makubaliano yaliyofikiwa ni kwamba Serikali itazinunua hisa asilimia 26 zilizokuwa zikimilikiwa na *Continental AG* ya Ujerumani katika Kiwanda hicho kwa Dola za Marekani milioni moja na

hivyo kuifanya Serikali kukimiliki Kiwanda cha General Tyre kwa asilimia 100.

42. ***Mheshimiwa Spika,*** baada ya hatua hiyo, sasa NDC inatarajiwa kuanza ukarabati wa mitambo na kufanya majaribio ya uzalishaji wa matairi na wakati huo huo ikitafuta wabia wenye uwezo na uzoefu wa uzalishaji matairi ya magari. ***Mheshimiwa Spika,*** naomba nitamke kuwa ufufuaji wa kiwanda hicho ni hatua nzuri katika kuongeza ajira kwa vijana wetu na hususan waliopo Jiji la Arusha, kupunguza ajali barabarani kwani umadhubuti wa matairi ya kiwanda hicho utaendelezwa. Aidha, uwekezaji huo utawezesha kufufuliwa kwa mashamba ya mpira ya Kihuhwi - Muheza na Kalunga – Kilombero. Tayari jumla ya hekta 510 zimepandwa mpira kati ya hekta 1,539 zilizopo. Aidha, kuna mpango wa kuanzisha mashamba mapya ya mpira ili kutosheleza mahitaji ya mpira hapa nchini.

4.4 Ufufuaji Kiwanda cha Kilimanjaro Machine Tools, Moshi

43. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2014/2015, Wizara kupitia NDC iliendelea kutekeleza hatua za kukifufua Kiwanda cha KMTC kilichopo Moshi kwa kukamilisha

ukarabati wa majengo ya utawala na miundombinu muhimu; kuandaa Mpango wa Kukifufua Kiwanda (*Turn around Business Plan*); kuendelea na utengenezaji wa vipuri na zana kwa ajili ya viwanda vya madini, saruji, kemikali na kilimo unaendelea; kujenga *"Mini-Foundry"* na baadaye kujenga *foundry* kubwa kwa ajili ya kukidhi mahitaji ya vipuri katika viwanda mbalimbali nchini na nje ya nchi kwa kutumia chuma cha Liganga kama malighafi.

4.5 Ujenzi wa Kiwanda cha Viuadudu –TAMCO (Kibaha)

44. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2014/2015, Wizara imekamilisha ujenzi wa Kiwanda cha Viuadudu vya Kuua Viluwiluwi vya Mbu wanaoeneza Malaria huko TAMCO, Kibaha, Mkoani Pwani. Hivyo, matarajio yetu ni kukabidhiwa na kuzinduliwa rasmi kwa Kiwanda na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, hapo tarehe 25 Juni, 2015. Teknolojia itakayotumika kuzalisha viuadudu ni ya kipekee Barani Afrika na hivyo viuadudu vitakavyozalishwa vitasaidia kuua mbu na kutokomeza ugonjwa wa malaria nchini na pia vitauzwa nje na kuliingizia Taifa fedha za kigeni takribani Dola za Marekani milioni 48.6 kwa

mwaka na ajira zipatazo 670. Kukamilika kwa Mradi huo kunatimiza azma ya Serikali ya Awamu ya Nne ilipoingia madarakani kuwa itachukua hatua madhubuti za kutokomeza malaria.

4.6 Uendelezaji Viwanda vya Nyama

45. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia, NDC imekamilisha upembuzi yakinifu wa kuanzisha viwanda vya kusindika nyama katika Mikoa ya Arusha, Dodoma, Mbeya na Pwani. Kwa sasa, mazungumzo na mamlaka mbalimbali yanaendelea kuhusu upatikanaji wa ardhi kwa ajili ya miradi hiyo. Utekelezaji wa miradi hiyo unafanywa kwa kushirikiana na Wizara ya Mifugo na Maendeleo ya Uvuvi na Kampuni ya Ranchi ya Taifa (NARCO).

4.7 Kilimo cha Michikichi na Usindikaji Mawese-Mkuranga

46. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara, kupitia NDC, imeanza utekelezaji wa miradi ya kilimo cha mashamba makubwa ya kibiashara sambamba na viwanda vya usindikaji mazao ya mashamba husika. Aidha, wawekezaji watawaunganisha wananchi wanaoyazunguka kama *Outgrowers.* Utaratibu huo umetumika

katika Kilimo cha Michikichi na Usindikaji Mawese huko Mkuranga, Mkoani Pwani, katika Mradi utakaotekelezwa kwa ubia kati ya NDC na Kampuni ya *Nava Bharat Ventures Limited* (NBV) ya Singapore. Mradi huo utatekelezwa katika shamba la hekta 10,000 kwa gharama ya Dola za Marekani milioni 111 kuzalisha lita milioni 58 za mafuta ya mawese kwa mwaka, umeme megawati 10, kuliingizia Taifa fedha za kigeni takriban Dola za Marekani milioni 51 kwa mwaka na ajira takriban 5,000. Utekelezaji wa mradi huo unategemewa kuanza mara baada ya kukamilisha taratibu za NDC kumilikishwa ardhi kiasi cha hekta 4,000 za awali katika kijiji cha Kimala Misale ambazo zimefikia hatua za mwisho.

4.8 Maeneo Maalumu ya Uwekezaji Chini ya EPZA

47. ***Mheshimiwa Spika,*** dhana ya Maeneo Maalum ya Uzalishaji kwa Mauzo Nje (EPZ) au Maeneo Maalum ya Uwekezaji (SEZ) inatekelezwa katika nchi nyingi duniani, ikiwemo Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na pia Jumuiya ya Kusini mwa Afrika. Dhana hii ndiyo chimbuko la mapinduzi ya viwanda nchini China kwani nchi hiyo imetekeleza mfumo huo kwa tija na faida kubwa. Kwa upande wa Tanzania, utekelezaji

ulianza mwaka 2006 kupitia Mamlaka mahsusi ya kusimamia na kuendeleza maeneo hayo. Tangu wakati huo, mafanikio makubwa yamepatikana. Mathalan, uwekezaji umekuwa ukiongezeka mwaka hadi mwaka, kutoka Dola za Marekani milioni 88 mwaka 2007 hadi kufikia Dola za Marekani milioni bilioni 1.3 mwaka 2014, sawa na ongezeko la asilimia 1,377 na jumla ya ajira za moja kwa moja kufikia 31,923.

48. ***Mheshimiwa Spika,*** ningependa kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa, kuanzia mwaka 2015/2016, Wizara kwa kushirikiana na Mamlaka ya EPZ, Sekta Binafsi na Taasisi za Fedha za ndani na nje ya nchi itaanza uendelezaji wa maeneo yaliyofidiwa, hata kama fidia husika haijafikia asilimia 100. Hatua hiyo itahusu Maeneo Maalum ya Uwekezaji yaliyotengwa katika mikoa ishirini (20) nchini. Mathalan, miradi itakayoendelezwa katika Mkoa wa Mtwara kwa mwaka 2015/2016 ni Kiwanda cha Mbolea; Mikoa ya Kigoma na Dar es Salaam ni ujenzi wa *Logistics Centres*; na Mkoa wa Pwani ni ujenzi wa Bandari ya Bagamoyo na Mitaa ya Viwanda vya Nguo na Mavazi. Wakati huohuo hatua za kutenga Maeneo Maalum katika mikoa mipya ya Geita, Katavi, Njombe, na Simiyu zinaendelea. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuongeza kasi ya utekelezaji mpango huo,

katika mwaka 2014/2015, Wizara ilijiwekea mkakati wa kushirikisha Sekta Binafsi katika kuendeleza maeneo hayo maalum. Kwa mfano, uendelezaji wa Bagamoyo SEZ unahusisha ubia wa utatu baina ya Tanzania, China na Oman, baada ya Serikali kuingia Mkataba wa Utatu *(Tripatite Agreement)* kati ya Kampuni ya *China Merchants Holdings International (CMHI)* na Serikali ya Oman kupitia Shirika lake liitwalo *State General Reserve Fund (SGRF).*

4.9 Uendelezaji Viwanda Vidogo na Ujasiriamali

49. ***Mheshimiwa Spika,*** uendelezaji Viwanda Vidogo, vya Kati na Biashara Ndogo na za Kati (SMEs) ndio mkakati pekee wa kujenga Kada ya Watanzania walio wengi Wanaviwanda na Wafanyabiashara wa Kati na Wakubwa. Katika kufikia azma hiyo, Wizara ilitekeleza mambo yafuatayo kwa mwaka 2014/2015: kuendelea kusimamia utekelezaji wa Sera ya Maendeleo ya Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo kwa kuweka mazingira mazuri ya ufanyaji na uzalishaji; kupanua wigo wa upatikanaji wa mitaji kupitia mifuko na dhamana za mikopo kwa masharti nafuu; ujenzi wa ujasiriamali kwa kutoa mafunzo kuhusu uongezaji thamani, ufungashaji bidhaa

na huduma za masoko kwa mazao ya kilimo na bidhaa nyingine ghafi; uhamasishaji wa Halmashauri za Miji na Wilaya kutenga maeneo ya Wajasiriamali Wadogo na Wakati ili kuendelea kuboresha mazingira ya uwekezaji na ufanyaji biashara. Aidha, Wizara imeanza kufanya marejeo ya Sera ya Maendeleo ya Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo kwa kushirikisha wadau ili sera hiyo iendane na mabadiliko ya kiuchumi na kijamii Kitaifa na Kimataifa.

50. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa biashara ndogo, Waheshimiwa Wabunge na Wananchi kwa jumla mtakumbuka kuwa changamoto inayowakabiri wafanyabiashara wadogo, maarufu kama ***Machinga*** au ***Nguvu Kazi*** au ***Mama Lishe*** ambao majirani zetu nchini Kenya na Uganda wanawaita ***Jua Kali*** ni uhaba wa maeneo mazuri ya kufanyia shughuli zao. Matokeo yake ni kwamba kundi hili la Wajasiriamali linaonekana kama kero kwa baadhi ya wananchi.

51. ***Mheshimiwa Spika,*** rai yangu kwa Waheshimiwa Wabunge, Viongozi na Wananchi wote ni kwamba hatunabudi kubadili mtazamo wetu kuhusu suala la Wajasiriamali hao. Mtazamo tulionao baadhi yetu ni kuwaona ***Machinga, Mama Lishe*** na ***Wajasiriamali***

wengineo wasio rasmi kuwa ni kero. Wizara, kwa kutambua umuhimu wa wajasiriamali wadogo wakiwemo ***Machinga, Mama Lishe*** na wengineo wasio rasmi imeendelea kutafuta ufumbuzi wa kudumu wa changamoto hiyo. Katika mwaka 2014/2015, Wizara imeshirikisha Tawala za Mikoa hasa zile zenye matatizo ya mara kwa mara. ikiwemo Mikoa ya Arusha, Dar es Salaam, Mbeya na Mwanza na kupata njia nzuri ya kupunguza na kama si kuondoa kabisa changamoto ya maeneo muafaka ya kufanyia kazi kwa wajasiriamali wadogo wakiwemo ***Wamachinga***.

52. ***Mheshimiwa Spika,*** kufuatia majadiliano hayo na maagizo ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Mizengo Peter Pinda, tayari baadhi ya Halmashauri zimeanza kutenga maeneo mahsusi ya Wamachinga. Mathalan, Mkoa wa Mwanza umeainisha maeneo yafuatayo kwa ajili ya Machinga: Mmilombo, Makoroboi, *Market Street,* na Stendi ya Zamani ya Mkwajuni. Aidha, wakati Mikoa inaendelea kutenga maeneo ya kudumu ya wajasiriamali wadogo na wamachinga ilikubalika kuwe na mipango ya muda mfupi na wa wakati, ambayo ni pamoja na kuanzisha magulio kwa kutumia barabara kwa saa na siku maalum. Mipango hiyo inafanyika kwa kushirikiana na Wizara ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Hivyo,

Mheshimiwa Spika, napenda kutumia fursa hii kurejea maagizo ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwanza kuacha kuwanyang'anya mali zao na pili kuhakikisha wanatengewa maeneo ya kufanyia biashara. Tatu, Wizara inaangalia utaratibu wa kuwapatia ***Machinga*** Leseni Maalum za kufanyia biashara zitakazo wafanya watambuliwe rasmi na mamlaka mbalimbali nchini ili kuondokana na bughudha wanayopata.

53. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuendeleza juhudi za Serikali katika ujenzi wa kada ya wajasiriamali walio madhubuti na endelevu, katika kipindi cha mwaka 2014/2015, Wizara iliwezesha jumla ya wajasiriamali 1,711 kupewa mikopo ya thamani ya shilingi bilioni 1.776 kupitia Mfuko wa Taifa wa Uendelezaji Ujasiriamali *(National Entrepreneurship Development Fund - NEDF).* Kati ya mikopo hiyo, asilimia 45 (kwa idadi) na asilimia 38 (kwa thamani) ilitolewa kwa miradi ya vijijini, na asilimia 52 (kwa idadi) na asilimia 46 (kwa thamani) ilitolewa kwa wanawake. Aidha, kupitia mikopo hiyo, jumla ya ajira 2,876 zilipatikana ambapo asilimia 51 ya ajira hizo zilikwenda kwa wanawake.

54. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuendesha Mfuko wa NEDF, Wizara imebaini kuwa baadhi

ya wadau wetu wamefikia viwango vya Ujasiriamali wa Kati (*Graduated to Medium Enterprises*) kiasi kwamba baadhi yao sasa wanakopesheka kwa masharti ya kawaida ya kibenki. Pamoja na mafanikio hayo, Wizara imebaini kuwa kiwango cha juu cha mkopo toka Mfuko wa NEDF, ambacho ni Shilingi milioni tano (5), hakikidhi mtaji wa kuanzisha viwanda, na hususan Viwanda vya Kati. Kwa mantiki hiyo, katika mwaka 2014/2015, Wizara kwa kushirikiana na Serikali ya Japani na CRDB imeanzisha Mfuko wa Dhamana ya Mikopo *(SME Credit Gurantee Scheme*) wenye mtaji wa shilingi 2 bilioni. Mtaji wa Mfuko huo umetolewa na Mfuko wa pamoja kati ya Serikali ya Tanzania na Japani *(Tanzania - Japani Food Aid Counterpart Fund na Japan International Cooperation Agency).* Wajasiriamali watakaokidhi masharti ya kukopeshwa wataunganishwa na Benki ya CRDB. ***Mheshimiwa Spika,*** rai yangu kwa wadau wetu ni kwamba waitumie fursa hiyo vizuri ili kuwapa imani Wabia wetu wa Maendeleo, ambao ni Serikali ya Japan iliioonesha nia ya kuongeza fedha katika Mfuko huo ili kuwawezesha Watanzania watakaofaulu katika uendeshaji wa viwanda vya kati wawezeshwe kuanzisha viwanda vikubwa. Hiyo ndiyo dhamira ya muda wa kati na mrefu ya Wizara ya Viwanda na Biashara.

55. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2014/2015 Mradi wa MUVI wa utoaji huduma kwa wajasiriamali vijijini nchini ulifanyiwa tathmin na kuonekana kuwa hadi sasa hatua mbalimbali za utekelezaji wake zimefikiwa kwa familia 92,910 (82% ya lengo) na kuzalisha ajira 13,026 (85% ya lengo), miradi 15,580 (89%) imeanzishwa na kuimarishwa. Aidha, uzalishaji wa wakulima 69,929 (89%) uliongezeka kutokana na huduma wanazopewa na mradi wa mlolongo wa uongezaji thamani katika mazao ya kilimo na malighafi nyinginezo. Mradi huo unatekelezwa katika Mikoa ya Ruvuma (Muhogo, Mahindi na Alizeti), Iringa (Nyanya, Serena na Alizeti), Pwani (Muhogo, Ufuta na Matunda), Tanga (Matunda, Maharagwe na Alizeti), Manyara (Mifugo na Alizeti) na Mwanza (Muhogo, Mpunga na Alizeti). ***Mheshimiwa Spika,*** kutokana na mafanikio makubwa yaliyopatikana katika utekelezaji wa Mradi wa MUVI, katika mwaka 2014/2015, Wizara iliweza kuomba na kukubaliwa kuongezewa muda wa mradi ili kuweza kukamilisha shughuli za mradi katika mikoa husika. Wadau wa Maendeleo wamekubali kuongeza muda wa utekelezaji kwa miaka miwili hadi Septemba, 2016. Aidha, Wizara imewaomba Viongozi wa Mikoa na Halmashauri kuuhuisha Mradi wa MUVI katika mipango yao ya maendeleo ili sasa Mpango huo

mzuri uweze kutekelezwa katika Mikoa yote chini ya ***Kauli Mbiu isemayo Wilaya Moja Zao Moja (One District One Product-ODOP).***

56. ***Mheshimiwa Spika***, kwa upande wa SIDO, kwa mwaka 2014/2015, Wizara ilianza kuchukua hatua za makusudi za kuimarisha na kuipa mwelekeo mpya kwa kutekeleza mambo yafuatayo:-

(a) Kuongeza idadi ya watumishi wa SIDO;

(b) Kuanzisha maeneo ambayo SIDO inayamiliki nchini na kuyaandalia mpango – kazi wa kuyaendeleza yenyewe au kupitia utaratibu wa PPP;

(c) Kuanza kujenga mitaa mipya ya viwanda (Industrial Parks) katika mikoa mipya, na

(d) Kuangalia uwezekano wa kuibadili SIDO ili iwe Mamlaka ya Uendelezaji Viwanda Vidogo na vya Kati Nchini.

4.10 Utafiti katika Uendelezaji Viwanda

57. ***Mheshimiwa Spika***, matumizi ya sayansi na teknolojia bora na ya kisasa hayaepukiki iwapo tunataka kuendelea kiviwanda haraka. Kimsingi, sayansi na teknolojia ndiyo mambo yanayozitofautisha nchi

changa kiuchumi na zile zilizoendelea. Hivyo, uendelezaji wa sayansi na teknolojia katika viwanda vyetu utalifanya Taifa kuhimili ushindani wa kibiashara katika soko la ndani, Kikanda na Kimataifa.

Hivyo**,** katika mwaka 2014/2015, Wizara iliendelea kuimarisha Taasisi zake za Utafiti, Maendeleo ya Teknolojia za TIRDO, TEMDO na CAMARTEC kama ifuatavyo:

TIRDO

(i) Kuwajengea uwezo wa kitaalam kuhusu nishati nchini India Wataalam husika hatimaye watumike katika tasnia ya nishati ya makaa ya mawe kwa matumizi ya viwanda vikubwa na vidogo, biashara, na pia majumbani;

(ii) Ujenzi wa maabara ambayo imekamilika kwa asilimia tisini (90%) itakayosaidia kujenga uwezo wa Taifa katika kukabiliana na uhalifu wa mtandaoni (*Cyber Security*) katika Taasisi za Serikali na Wakala wa Serikali;

(iii) Kujenga uwezo wa kutoa mafunzo ya kuchakata taka za ngozi (leather recycling machine) ambapo mtambo wa kufundishia taaluma hiyo umenunuliwa na kusimikwa kwa asilimia tisini (90%);

(iv) Kuendelea kuhakiki (Accreditation) na kuboresha maabara ya mazingira na ya vifaa vya kihandisi ili ziweze kufikia viwango vya kimataifa katika kutoa huduma bora kwa wazalishaji viwandani nchini ikiwemo Sekta ya Gesi Asilia; na

(v) Kuendelea kutoa msaada wa kitaalam kwa Kampuni ya GS1 kutekeleza kazi ya ufuatiliaji wa mazao (traceability) ambapo hadi kufikia mwezi Aprili, 2015 jumla ya bidhaa 13,750 zimepatiwa nembo za mstari na kampuni 815 zimekuwa wanachama wa GS1 hapa nchini, kati ya hizo, kampuni nne (4) ni kutoka nje ya Tanzania.

CAMARTEC

(i) Kubuni na kutengeneza chasili(Prototype) ya Trekta Dogo na Mashine ya Kupura aina mbalimbali za nafaka;

(ii) Mashine ya kufunga majani kwa ajili ya kuboresha matumizi ya malisho kwa ajili ya kuongeza muda wa upatikanaji wa malisho imebuniwa na tayari mashine tatu za aina hiyo zimeuzwa Mkoani Dodoma na Kilimanjaro;

(iii) Kujenga mitambo ya biogesi kwa kushirikiana na Wizara ya Nishati na Madini katika magereza ya Kiabakari,

Butimba, Mugumu, KPF Mkoani Morogoro, Ubena Mkoani Pwani na King'anga Mkoani Dodoma utakamilishwa mwaka 2015/2016;

(iv) Majiko ya biogesi 1,000, viunganishi vya mitambo ya biogesi 1,000 na vifaa mbalimbali vya nishati ya biogesi vimesambazwa kwa watumiaji katika Mikoa ya Arusha Dodoma, Kagera, Kilimanjaro, Manyara, Mara, Mwanza, Singida na Tanga;

(v) Mafunzo kwa zaidi ya Mafundi Waashi 800, Wasimamizi 400, na watumiaji zaidi ya 15,000 wa teknolojia ya biogesi kupitia miradi ya Kituo; ujenzi wa mitambo, usimamizi na udhibiti wa ubora na matumizi mazuri ya teknolojia ya biogesi. Aidha, mazungumzo yameanza na Wizara ya Mifugo ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kuhusu ujenzi wa mitambo ya biogesi huko Zanzibar.

TEMDO

(i) Imekamilisha kubuni na kutengeneza chasili (prototype) ya mtambo wa kuzalisha umeme (micro hydro power plant) vijijini na majaribio ya mtambo huo yanaendelea katika karakana ya TEMDO;

(ii) Imekamilisha ubunifu wa utengenezaji kibiashara wa mtambo wa kusindika na kusafisha mafuta yatokanayo na mbegu za mimea (oil expelling and refining plant). Tayari wajasiriamali wawili waliopo katika Mkoa wa Dodoma wanatumia mtambo huo kwa majaribio. Aidha, uhawilishaji wa teknolojia hiyo unaendelea kufanyika kupitia wajasiriamali watengenezaji (Small manufacturing enterprises);

(iii) Kuhamasisha utengenezaji wa mitambo ya kuteketeza taka za hospitali (health care waste incinerator) kibiashara kupitia wajasirimali watengenezaji unaendelea;

(iv) Imebuni na kusanifu jokofu la kuhifadhia vifaa vya hospitali pamoja na maiti (refrigeration systems for medical use including mortuary facility) na kazi ya kutengeneza chasili (prototype) inaendelea;

(v) Imebuni na kusanifu mitambo ya kibiashara ya kutengeneza kuni au mkaa kutokana na mabaki ya mimea (Biomass briquetting plant). Uhawilishaji wa mitambo hiyo umefanyika kwa wajasiriamali watatu (3) katika mikoa ya Arusha na Dodoma;

(vi) Imekamilisha ubainishaji wa mahitaji ya teknolojia na huduma za kihandisi katika

viwanda na sekta nyingine nchini na utoaji wa huduma unaendelea; na

(vii) Imetoa huduma za ushauri wa kihandisi viwandani kwa viwanda 7 vya *A to Z Textile Mills Ltd, Kijenge Animal Products, Arusha Coffee Millers, Mount Meru Millers, TBL* Arusha na Minjingu *Mining and Fertilizer Company* katika mikoa ya Arusha na Kilimanjaro. Aidha, utoaji wa huduma hiyo unaendelea katika mikoa mingine.

4.11 Ujuzi na Weledi katika Uzalishaji Viwandani

58. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara kwa kushirikiana na Benki ya Dunia imekamilisha utafiti ili kubaini kwanini bidhaa kutoka nje na hususan kutoka kwa washindani wetu kama China huuzwa nchini, na kwa kweli Afrika Mashariki yote, kwa bei ya chini ikilinganishwa na bidhaa za Tanzania. ***Mheshimiwa Spika***, katika utafiti huo Wizara ilichukua uamuzi wa makusudi kabisa kujilinganisha na Jamhuri ya Watu wa China, Taifa namba mbili kiuchumi duniani na linalotoa chagizo hata katika masoko ya nchi zilizoendelea duniani. Hatukutaka kujilinganisha na mataifa yanayoendelea hata kama yametuzidi kidogo kiviwanda kwa sababu tunaamini kabisa kwamba mtu binanfsi au Taifa likitaka kupiga hatua kubwa ya kimaendeleo

budi lijipime na washindani walio bora kabisa duniani. Mathalan, katika medani ya riadha, mkimbiaji makini hujipima kasi yake na rekodi ya dunia. Vivyo hivyo, katika uendelezaji viwanda, Wanaviwanda wetu budi watumie teknolojia ya kisasa kabisa ili uzalishaji wao uwe wenye tija na bidhaa zenye viwango vya kimataifa. Hiyo ndiyo njia pekee ya kukabiliana na ushindani wa Kikanda na Kimataifa.

59. ***Mheshimiwa Spika***, katika utafiti huo imeabainika kuwa gharama za ajira kwa Tanzania ziko chini ikilinganishwa na viwango vya mishahara wanayolipwa wafanyakazi viwandani nchini China. Jambo ambalo China wanatuzidi ni katika ujuzi na weledi wa wafanyakazi wao viwandani (*Skilled Manpower*) na pia wanahamasa zaidi ya kufanyakazi (*Highly Motivated*). Miongoni mwa motisha wanazopewa ni huduma za makazi jirani na kiwanda alichoajiriwa. Hivyo, mtumishi halazimiki kusafiri kwa gari au kwa njia nyingine yoyote ile kwenda kazini. ***Mheshimiwa Spika***, kwa kutambua changamoto ya ukosefu wa watumishi wenye ujuzi viwandani, Wizara imeanza kuchukua hatua za kuitatua kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu na Ufundi, na hususan VETA.

4.12 Ujuzi na Weledi katika Biashara

60. ***Mheshimiwa Spika***, dhana ya biashara imegawanyika katika makundi mawili makuu, yaani biashara ya bidhaa, ambayo sote tunaifahamu, na kisha biashara ya huduma. Itakumbukwa kuwa baada ya Uhuru, Serikali ilianzisha vyuo mahsusi vya kufunza taaluma ya biashara. ***Mheshimiwa Spika,*** napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa biashara ya huduma inahitaji ujuzi na weledi wa hali ya juu zaidi ikilinganishwa na biashara ya bidhaa. Mathalan, kwa upande wa Tasnia ya Utalii, kuna Chuo kimoja tu Afrika Mashariki kilichobobea katika fani hiyo, nacho ni *Utalii College.* VETA wamejaribu kuziba ombwe hilo kwa kufungua chuo cha aina hiyo Jijini Arusha. Hivyo, kwa upande wa Wizara yangu, hatua zimechukuliwa kwa mwaka 2014/2015 kuongeza huduma za Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE) ili kuwafikishia wananchi wengi zaidi mafunzo ya Elimu ya Biashara. Mathalan, Chuo kimepata eneo lenye ukubwa wa ekari 54.9 huko Iganzo, Mbeya ili kujenga Madarasa, Ofisi, Kumbi za Mihadhara na Maktaba kwa Kampasi mpya ya Mbeya; Chuo kinaandaa Mpango Kabambe (Master Plan) wa upanuzi wa miundombinu katika Kampasi ya Dar es salaam na ujenzi wa Kumbi za Mihadhara, Hosteli pamoja na Ofisi za Wakufunzi kwa Kampasi ya

Dodoma na Mwanza; Chuo kipo katika utafiti wa masoko (Market Survey) kujua aina ya mitaala yenye tija ili kuendana na mahitaji ya soko la ajira ikiwemo fani ya nishati ya mafuta na gesi na mitaala mipya katika ngazi ya uzamili (Master's Degree); na mchakato wa kuandaa mtaaala wa ujasiriamali na elimu ya biashara ya kisasa unaendelea.

4.13 Sensa ya Viwanda

61. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS) inaendelea na Sensa ya Viwanda nchini baada ya kukamilika kwa zoezi la uorodheshaji viwanda. Ni dhahiri kuwa kazi hiyo ni kubwa na itaigharimu Serikali fedha nyingi lakini itasaidia kupatikana kwa takwimu mbalimbali za Sekta ya Viwanda na hivyo kuwezesha Serikali kuwa na mipango na maamuzi sahihi ya kutatua changamoto mbalimbali zinazokabili viwanda vyetu. Aidha, shughuli zilizofanyika ni pamoja na: Kufanya *"Pilot Survey"* ya zoezi la ukusanyaji wa takwimu za kina za Sensa ya Viwanda nchini; Kufanya mafunzo ya Wakufunzi, Wadadisi na Wasimamizi kwa lengo la kuwandaa kukusanya taarifa za kina viwandani. Zoezi la ukusanyaji wa takwimu za kina nchi nzima limeanza mwezi Machi, 2015 na linatarajia kukamilika mwezi Juni, 2015.

Wizara pia, itatumia fursa hiyo ya zoezi la sensa katika kufanya tathmini ya maendeleo ya viwanda ambapo changamoto mbalimbali zinazoikabili Sekta ya Viwanda zitabainishwa na hatimaye kutafutiwa ufumbuzi wake.

4.14 Programu Mahsusi za Kuongeza Tija na Ufanisi Viwandani

62. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuongeza tija Viwandani, Wizara imeendelea kutoa mafunzo ya kuongeza tija, ufanisi pamoja na ubora wa bidhaa kwa wenye Viwanda kupitia Programu ya *Kaizen* kwa kushirikiana na Shirika la Misaada la Japan (JICA) pamoja na UNIDO. Katika kipindi cha mwaka 2014/2015, jumla ya viwanda 42 vilivyopo katika mikoa ya Dar es Salaam, Dodoma na Morogoro vimejiunga na Mradi wa *Kaizen* na kupatiwa mafunzo ya nadharia na vitendo. Mradi pia, umeanzisha uhusiano wa kimataifa wa kupeana taarifa za maendeleo ya mradi wa *Kaizen* kwa nchi zinazotumia dhana hiyo, kwa mfano, Kenya na Sri-Lanka. Vilevile, Wizara kwa kushirikiana na UNIDO imeendelea kutoa mafunzo ya kuongeza tija, ufanisi pamoja na ubora wa bidhaa za viwandani kupitia Mradi wa Kuboresha Ufanisi wa Viwanda (*Tanzania Industrial Upgrading and Mordenization Project*). Katika kipindi cha

mwaka 2014/2015, mafunzo ya kiufundi ya kuongeza ufanisi na ubora wa bidhaa yalitolewa kwa viwanda 15 katika Sekta Ndogo za Maziwa, Mafuta ya Alizeti, nafaka na matunda katika Mkoa wa Dodoma. Aidha, Mradi umeanzisha Kongano (Cluster) ya viwanda vya Mafuta ya Alizeti katika Wilaya ya Chamwino ambapo tayari Manispaa ya Dodoma imeshatoa ardhi ya kuanzisha Kongano.

4.15 Uendelezaji Viwanda Kikanda

63. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kushiriki katika uhamasishaji wa utekelezaji wa Mpango Kazi wa Sera ya Viwanda ya Jumuiya ya Afrika Mashariki na Mkakati wa Uendelezaji Viwanda kwa nchi za SADC. Katika kipindi cha mwaka 2014/2015, Wizara imeshiriki kikamilifu katika kuandaa na kukamilisha Mpango Kazi wa Sera ya Viwanda ya Jumuiya ya Afrika Mashariki; na Mkakati na Mpango Kazi wa Maendeleo ya Viwanda kwa Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC) uliozinduliwa na Viongozi Wakuu wa SADC tarehe 29 Aprili, 2015 huko Harare, Zimbabwe.

5.0 SEKTA YA BIASHARA NA MASOKO

5.1 Sekta ya Biashara

5.1.1 Mafanikio katika Sekta ya Biashara

64. ***Mheshimiwa Spika,*** Sekta ya Biashara imeendelea kupata mafanikio makubwa mwaka hadi mwaka. Mathalan, Sekta hiyo *ilikua kwa asilimia 10 mwaka 2014 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 4.5* mwaka 2013, ambayo ni sawa na ongezeko la asilimia 5.5. Ongezeko hilo lilitokana na mauzo ya bidhaa za kilimo na za viwandani na pia manunuzi ya bidhaa toka nje na hususan magari na pikipiki.

65. ***Mheshimiwa Spika,*** kulingana na takwimu za Sekretarieti ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, mauzo ya Tanzania katika Soko la Jumuiya ya Afrika Mashariki yameongezeka kutoka Dola za Marekani milioni 158.8 kwa mwaka 2012/2013 hadi kufikia Dola za Marekani milioni 723 kwa mwaka 2013/2014 sawa na ongezeko la asilimia 455.3. Aidha, mauzo ya bidhaa kwenye masoko mengine ya upendeleo katika ushuru wa forodha yaliongezeka, kwa mfano; mauzo kwenye soko la China yaliongezeka kutoka shilingi bilioni 176.8 mwaka 2012 hadi shilingi trilioni 1.13 mwaka 2014, sawa na ongezeko la asilimia 539. Vilevile,

mauzo ya bidhaa zetu yaliongezeka katika soko la India, kutoka shilingi bilioni 90.1 mwaka 2012 hadi shilingi bilioni 207.4 mwaka 2014, sawa na ongezeko la asilimia 130.

5.1.2 Sera na Mikakati ya Ukuzaji na Uendelezaji Mauzo Nje

66. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara, katika mwaka 2014/2015, ilianza kufanya mapitio ya Sera ya Biashara ya Taifa ili kuzingatia mabadiliko ya kibiashara yanayoletwa na utandawazi. Pamoja na mapitio hayo, Wizara imekuwa ikitekeleza mikakati mbalimbali iliyoainishwa katika sera hiyo hususan uongezaji tija na ufanisi katika uzalishaji na utoaji huduma; kuendeleza na kudumisha ushiriki wa Tanzania katika Jumuiya za kikanda na kupanua wigo wake kama inavyofanyika sasa kwa kuunda Ubia wa Utatu wa Ushirikiano wa Kiuchumi baina ya COMESA-EAC na SADC; kutumia njia za kujihami kiuchumi kupitia sera za fedha na kodi, kuendelea kuvutia wawekezaji kupitia EPZA, NDC, TIC na majukwaa mengine ya uhamasishaji uwekezaji; na kuhimiza uuzaji nje wa bidhaa zilizosindikwa badala ya bidhaa ghafi.

67. ***Mheshimiwa Spika***, pamoja na kutekeleza mikakati hiyo ya kukuza na kuendeleza mauzo nje, mwaka 2014/2015,

Wizara kwa kushirikiana na Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (TanTrade), Vituo vya Biashara London na Dubai, ilitekeleza mambo yafuatayo:

(a) Kuandaa Maonesho ya 38 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam, maarufu kama Sabasaba, yaliyofanyika kuanzia tarehe 28 Juni, - 8 Julai, 2014 katika Uwanja wa Maonesho wa Mwl. J.K. Nyerere, yakivutia makampuni 1,750 ya ndani na 500 kutoka nchi 32 yalishiriki;

(b) Kuratibu na kushiriki maonesho mbalimbali ya kimataifa kama ifuatavyo: *Nairobi International Trade Fair, 2014,* Kenya yakishirikisha wajasiriamali 5 kutoka Tanzania; Maonesho ya Chakula na Huduma ya Oman (Oman Expo 2014) ambapo Kampuni zaidi ya 15 zilijitokeza kutaka uwakala wa kusambaza chai na kahawa kutoka Tanzania; Maonesho ya Kimataifa ya Swaziland ambapo wajasiriamali 6 kutoka nchini walishiriki; Maonyesho ya Nguvu Kazi/Juakali, Kigali, Rwanda na Maonesho ya Kimataifa ya Msumbiji ambapo wajasiriamali 4 walishiriki kutoka nchini; Maonesho ya *Expo 2015 Milan Italia*. Maonesho hayo yaliyoanza tarehe 1 Mei

mwaka huu yataendelea hadi tarehe 31 Oktoba 2015 yakijumuisha nchi 149.

68. ***Mheshimiwa Spika,*** mbinu nyingine iliyotumiwa na Wizara mwaka 2014/2015 katika kukuza mauzo nje ni kupitia vituo vyake vya Biashara vya Dubai na London kama ifuatavyo:

5.1.3 Kituo cha Biashara cha Tanzania Dubai (TTC-DUBAI)

(a) Kituo kwa kushirikiana na TAHA, kimeendelea kuandaa ziara za mauzo kwa bidhaa za matunda na mboga mboga ili kuongeza mauzo ya bidhaa hizo kufuatia kuongezeka kwa safari za ndege kati ya Tanzania na Falme za Kiarabu (UAE) ambapo sasa Shirika la Ndege la Emirates wameanzisha safari mbili za ndege kwa siku, *Fly Dubai* wameanzisha safari moja ya ndege kila siku; na *Etihad* wameanza safari za ndege ya mizigo. Ongezeko hilo limewezesha kushuka kwa gharama za kusafirisha mizigo. Hii imesaidia kuongeza ushindani kwa bidhaa zetu kwenye soko la UAE;

(b) Kituo kwa kushirikiana na Kampuni ya *National Bee Keeping Supplies* kiliwezesha makampuni ya Tanzania kushiriki kwenye

maonesho ya Chakula (*Gulfood)* yaliyofanyika tarehe 8-12 Febrauri, 2015. Bidhaa zilizooneshwa katika maonesho hayo ni pamoja na asali, maparachichi, nyama, nazi, madafu, chai, karafuu, tangawizi kavu, pilipili manga, embe, mbegu za mlonge na kahawa na kupata maulizo ya bidhaa hizo ya Dola za Marekani milioni 15 ambayo yanafanyiwa kazi kwa kushirikiana na *National Bee keeping Supplies Limited*, *Fursa Export House, Rungwe Avocado Company*, *Makai Moringa Enterprises* na wanachama wa *Tanzania Mango Growers Association;*

(c) Kituo kwa kushirikiana na Ubalozi Mdogo na Wadau wa Sekta ya Utalii nchini kiliandaa kongamano la uwekezaji kwenye *Real Estate* na miumdombinu mingine ya Utalii na Biashara ya Utalii lililofanyika mwezi Disemba, 2014 mjini Dubai ambapo Mgeni Rasmi alikuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Mizengo Peter Pinda. Kufuatia kongamano hilo, Kampuni ya *Radisson* ya USA imeonesha nia ya kuwekeza katika hoteli ya nyota tano jijini Dar es salaam; na

(d) Kituo kimeendelea kutoa taarifa kwa wafanyabiashara wa UAE kuhusu

matumizi ya njia sahihi za kuagiza madini kutoka Tanzania hali ambayo imesababisha kuongezeka kwa mauzo ya bidhaa za Tanzania kwenye soko la UAE kufikia Dirham bilioni 4 mwaka 2014 ikilinganisha na Dirham milioni 500 mwaka 2007.

5.1.4 Kituo cha Biashara cha Tanzania London (LTC)

(a) Kituo, kwa kushirikiana na Ubalozi, kiliandaa Mkutano wa Wafanyabiashara wa Kitanzania na Mtaalam wa masuala ya biashara anayesimamia utekelezaji wa Programu ya Kimataifa (ITC) kwa lengo la kuangalia jinsi gani Watanzania walioko nje ya nchi (Diaspora business community) wanavyoweza kuchangia maendeleo ya Taifa;

(b) Kituo kwa kushirikiana na Wizara ya Maliasili na Utalii na Bodi ya Utalii (TTB), kilifanikisha ushiriki wa Tanzania katika maonesho ya Kimataifa ya Utalii Duniani, yajulikanayo kama *World Travel Market (WTM 2014).* Kituo vilevile kiliweza kuratibu ushiriki wa Maonesho ya Utalii yanayofanyika nchini Uingereza kama yale ya Manchester na London; na

(c) Kituo kiliiwakilisha nchi kwenye mikutano ya mashirika ya Kimataifa ambayo Tanzania ni nchi mwanachama, ikiwemo Shirika la Kimataifa la Kahawa Duniani (*International Coffee Organisation – ICO*), Shirika la Kimataifa la Sukari – ISO, Shirika la Katani – LSA, na Shirika la Kimataifa la Taaluma ya Kilimo - CABI. Hatua hiyo iliwezesha maslahi ya Taifa kulindwa na pia kupunguza gharama za ushiriki.

5.2 Sekta ya Masoko

5.2.1 Soko la Mazao na Bidhaa (Commodity Exchange)

69. ***Mheshimiwa Spika,*** ukombozi wa mkulima, wakiwemo wakulima wa Tanzania, unategemea sana kuwepo kwa mfumo wa soko ulio shindani na wa haki. Kitaifa, tumekuwa tukikabiliwa na changamoto ya bei ndogo kwa wakulima wetu kutokana na tija ndogo katika uzalishaji na hasa ukiritimba katika soko. Katika kukabiliana na changamoto ya soko lisilotoa bei ya haki kwa mkulima, Wizara yangu ilianzisha Mfumo wa Stakabadhi ya Ghalani. Katika mwaka 2014/2015, Wizara yangu, kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, imeandaa

Muswada wa Sheria ya kuanzisha Soko la Mazao na Bidhaa Nchini (Capital Market and Commodity Exchange Bill 2014), ambapo Waraka wake unasubiri kuwasilishwa katika Baraza la Mawaziri kabla ya kupelekwa Bungeni kwa ajili ya kupitishwa. Baadhi ya hatua zilizofikiwa hadi sasa za uanzishwaji wa soko hilo ni pamoja na usajili wa Kampuni itakayosimamia uendeshaji wa Soko hilo inayoitwa *Tanzania Mercantile Exchange Public Limited Company*. Kampuni hiyo itamilikiwa kwa ubia kati ya Sekta Binafsi kwa asilimia 51 ya hisa na Sekta ya Umma itakayomiliki asilimia 49 ya hisa zote. Ofisi zake zinatarajiwa kuwa katika Jengo la LAPF Makumbusho, Kinondoni, Dar es salaam. Katika ofisi hizo kutakuwa na *Electronic Platform Exchange* kwa ajili ya uuzaji wa mazao na bidhaa kwa mfumo wa kielekroniki. Vilevile, timu ya wataalamu ilienda Ethiopia, China na India kupata uzoefu wa uendeshwaji wa Soko la Mazao na Bidhaa. Sambamba na hatua hizo, Hadidu za Rejea (TOR) za kumpata Mshauri Mwelekezi wa kuandaa Mpango wa Biashara (*Business Plan*) zimeandaliwa, pamoja na Hadidu za Rejea za kumpata Mshauri Mwelekezi atakayeweza kubainisha upungufu uliopo kati ya Mfumo wa Stakabadhi Ghalani na Soko la Mazao na Bidhaa.

70. ***Mheshimiwa Spika***, mazao yatakayoanza kuuzwa kwenye soko hili ni korosho, kahawa, alizeti, mahindi na mchele. Aidha, bidhaa nyingine zitakazohusika ni zile zisizo za kilimo kama vile chuma, makaa ya mawe, madini na mafuta kwa kipindi cha baadae mfumo utakapokuwa umepata mafanikio makubwa katika uendeshwaji wake.

5.2.2 Miundombinu ya Masoko

71. ***Mheshimiwa Spika***, katika kuendelea kushirikiana na wadau ili kuendeleza miundombinu ya masoko nchini mwaka 2013/14, Wizara iliwezesha jumla ya masoko matatu kujengwa na kukamilika ambayo ni pamoja na Soko la Mkenda (Wilaya ya Songea Vijijini) katika mpaka wa Tanzania na Msumbiji, Soko la Mtambaswala (Wilaya ya Nanyumbu) katika mpaka wa Tanzania na Msumbiji, na Soko la Nyamgali (wilaya ya Buhigwe) katika mpaka wa Tanzania na Burundi. Ujenzi huo ulifanyika kwa kushirikiana na Mfuko wa Maendeleo wa Jumuiya ya Ulaya. Katika mwaka 2014/2015 Wizara ya Viwanda na Biashara imekabidhi rasmi soko la Nyamgali kwa Halmashauri ya Wilaya ya Buhigwe, Masoko ya Mkenda na Mtambaswala yapo katika hatua za mwisho za kukabidhiwa na kufunguliwa.

72. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha kuwa kunakuwa na uwazi na ushindani wa haki katika biashara, Wizara imeendelea kukusanya, kuchambua, kuhifadhi na kusambaza taarifa za masoko kwa mazao ya chakula na mifugo katika masoko mbalimbali nchini kwa wadau kwa wakati. Taarifa hizo husambazwa kwa wadau kupitia magazeti ya kila siku, ujumbe wa simu za kiganjani na tovuti ya LINKS ambayo ni *www.lmistz.net.*

5.2.3 Uboreshaji wa Mazingira ya Ufanyaji Biashara

73. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara imeendelea kukamilisha marekebisho ya sheria zinazokinzana na uboreshaji wa mazingira ya biashara kwa kuirekebisha Sheria ya Usajili wa Shughuli za Biashara (*The Business Activities Registration Act*– BARA ya mwaka 2007). Hati ya kuwasilisha marekebisho hayo Bungeni imeandaliwa. Aidha, katika mwaka 2014/2015, Wizara, chini ya Mpango wa Matokeo Makubwa Sasa (BRN), imeanza kuzifanyia marekebisho makubwa huduma zinazotolewa na Msajili wa Makampuni ili zitolewe kwa Mtandao, yaani TEHAMA. Hivi sasa Usajili wa Majina ya Biashara unafanyika kwa mtandao na Cheti kutolewa siku hiyo hiyo. Hivyo, mwananchi halazimiki kusafiri, mathalan toka Kigoma,

Mtwara na Kisarawe kwenda BRELA kusajili Jina. Hatua itakayofuata na ambayo tumeanza kuifanyia kazi ni Usajili wa Makampuni na Uwekaji Kumbukumbu za Shughuli ya Kampuni *(Company Registration and Filing Returns*). Vilevile, Wizara imeendelea kutoa taarifa kwa Wadau wake zinazohusu masuala ya Sekta ya Viwanda, Biashara na Masoko kupitia Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) katika kuimarisha na kuboresha huduma zake kupitia TEHAMA, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Wakala wa Serikali Mtandao imekamilisha mchakato wa kumpata Mtaalamu Mwelekezi atakayetengeneza Mfumo na Mtandao wa Tovuti ya Biashara ya Kitaifa (National Business Portal). Hatua inayosuburiwa sasa ni Kibali kutoka Benki ya Dunia ili taratibu za kumruhusu Mtaalamu huyo kuanza kazi ziendelee.

5.2.4 Usimamizi wa Sheria na Taratibu

74. ***Mheshimiwa Spika,*** uzingatiaji Sheria na Taratibu ni mambo muhimu sana katika kukuza na kuendeleza viwanda na biashara katika Taifa lolote lile. Hoja hiyo ndiyo sababu ya msingi ya Wizara yangu kuwa na Taasisi kadhaa za kusimamia sheria na taratibu za kibiashara na kiuchumi. Taasisi hizo

zimeainishwa katika **Jedwali Na. 1** na majukumu yake.

75. ***Mheshimiwa Spika,*** itakumbukwa kuwa katika kipindi kirefu kumekuwepo changamoto ya kuingizwa nchini hata kuzalishwa nchini bidhaa zisizokidhi viwango vya ubora; wafanyabiashara kutotumia vipimo sahihi vya uzito na ujazo na badala yake kutumia mtindo wa "Lumbesa" ambao umeshamiri; baadhi ya wafanyabiashara na wazalishaji kujaribu kutumia mbinu za kibiashara zisizo halali; na kunakili au kurudufu kazi za wasanii bila ridhaa yao au kulipia mrabaha unaostahili. Bidhaa hafifu zina athari kuu tatu katika uchumi wa Taifa: kwanza huhatarisha afya za walaji au watumiaji wa bidhaa husika; pili hudhoofisha uchumi wa nchi kwa kuwa Wananchi na Serikali hujikuta ikinunua bidhaa kwa gharama kubwa lakini zinazodumu kwa kipindi kifupi sana; na tatu mara nyingi bei ya bidhaa hafifu huwa ni ndogo na hivyo kusababisha ushindani usio wa haki kati ya bidhaa za aina moja lakini zilizotofautiana kwa ubora.

76. ***Mheshimiwa Spika,*** napenda kutumia fursa hii kuwataarifu Waheshimiwa Wabunge na Wananchi kwa jumla kuwa mtindo wa "*Lumbesa"* hauna mshindi baina ya mkulima na

mfanyabiashara. Mfanyabiashara kwa kujaziwa, mathalan gunia au kiroba hadi juu hudhani kapata. Si kweli! ***Mheshimiwa Spika***, ukweli ni kwamba Mkulima baada ya kunyonywa na ***Lumbesa*** kwa muda mrefu hupata welevu na kubuni njia za kukabiliana na hali hiyo. Mathalan, iwapo ni muuza viazi vya mviringo, anachofanya ni kuweka chini ya gunia viazi vyenye ukubwa mdogo sana na wakati mwingine matakataka tu na juu kwenye "Lumbesa" ndiko anakoweka viazi vikubwa na vizuri. Mfanyabiashara anaposafirisha viazi hivyo, mathalan, hadi Soko la Kariakoo hujikuta ana nusu gunia tu la viazi halisi. Pamoja na kudanganywa huko ajabu ni kwamba mtindo huo wa "Lumbesa" umeendelea na kuwa utamaduni wa Taifa. Kwa bahati mbaya udanganyifu huo umeanza kuingia katika biashara ya Kimataifa kiasi cha kutaka kuharibu sifa za baadhi ya wafanyabiashara wetu au bidhaa zetu katika medani ya Kimataifa. Sote tunajua jinsi watu wanavyoweka mawe kwenye pamba, mchanga kwenye ufuta n.k.

77. ***Mheshimiwa Spika,*** nimeonelea nichukue dakika hizo chache kuelezea madhara ya bidhaa hafifu na vipimo visivyo rasmi katika uchumi. Nimefanya hivyo kwa sababu Wizara na Taasisi zake za TBS na VIPIMO katika mwaka

2014/2015 zimechukua hatua madhubuti katika kukabiliana na hali hiyo. Hivyo, ***Mheshimiwa Spika***, naliomba Bunge lako Tukufu na Wananchi kwa jumla kuunga mkono hatua zinazochukuliwa sasa na Wizara yangu. Bila ya msaada wa Viongozi wa kisiasa na Serikali kwa jumla hatuwezi kushinda vita hiyo.

78. ***Mheshimiwa Spika,*** katika muktadha huo naomba nianishe utekelezaji kwa mwaka 2014/2015 kuhusiana na ubora wa vipimo na ushindani kwa kibiashara kama ifuatavyo:-

79. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuendelea kuimarisha usimamizi wa matumizi ya vipimo vilivyo sahihi, Wizara kupitia Wakala wa Vipimo imeendelea na kazi yake ya kusimamia, kuhakiki na kukagua vipimo mbalimbali kama nilivyodokeza katika utangulizi wangu ili kuhakikisha kuwa vipimo vinavyotumika nchini ni sahihi. ***Mheshimiwa Spika***, jambo la kutia moyo ni kwamba, utendaji wa Mamlaka katika kuhudumia Wananchi umeimarika sana. Mathalan, katika nusu ya mwaka 2014/2015, Wakala wa Vipimo imehakiki vipimo 286,919, ikiwa ni ongezeko la asilimia 5 ikilinganishwa na lengo la kuhakiki vipimo 274,556 hadi kufikia Desemba, 2014; na kaguzi 1,196 za vipimo mbalimbali zimefanyika kwa kuvuka lengo kwa asilimia 84. Aidha, Wizara imeendelea

kuimarisha Kitengo cha Vipimo Bandarini (WMA Ports Unit) chenye jukumu la kusimamia, kuhakiki na kukagua usahihi wa vipimo vitumikavyo kupimia kiasi cha mafuta yaingiayo nchini ili kudhibiti ukwepaji kodi.

80. ***Mheshimiwa Spika,*** kuhusu Tume ya Ushindani, Wizara imeendelea kujenga uwezo wa Sekretarieti ya Tume na Baraza kwa kuimarisha ujuzi na weledi wa rasilimali watu na Wajumbe wa Baraza ili kuweza kusimamia kwa ufanisi na weledi usawa na haki katika ufanyaji biashara. Katika mwaka 2014/2015, Baraza lilitarajia kusikiliza na kuamua kesi 24 za rufaa zinatokana na mchakato wa Udhibiti na Ushindani wa Biashara kwenye soko kutoka kesi 20 za mwaka 2013/2014. Hadi kufikia Februari, 2015 kulikuwa na kesi 24 zilizosajiliwa. Kati ya hizo, kesi 5 zimesikilizwa na kutolewa maamuzi, kesi 11 zimesikilizwa na zinasubiri hukumu wakati kesi 8 ziliendelea kusikilizwa. Changamoto kuu ya Baraza ni ucheleweshaji au kutotolewa fedha kabisa na taasisi zinazowajibika kisheria kufanya hivyo**.** Baraza na Wizara wanaendelea kujadiliana na Hazina kutafuta ufumbuzi wa kudumu dhidi ya ufinyu wa bajeti ya Baraza.

81. ***Mheshimiwa Spika,*** katika utangulizi wangu nimeelezea mafanikio ya kupigiwa mfano

yaliyofikiwa na Shirika la Viwango la Tanzania (TBS) katika mwaka 2014/2015. Kwanza, mwelekeo wa upimaji ubora wa bidhaa zote mahali zinapotoka kabla ya kuingia nchini (Pre-shipment Verification of Conformity to Standards -PVoC) umeimarika sana. Kwa kipindi cha miezi sita tu ya mwanzo wa mwaka 2014/2015, jumla ya vyeti vya ubora (Certificate of Conformity - CoCs) 15,304 vimetolewa. Mafanikio hayo yanatokana na hatua ya TBS kuhakikisha inashirikiana kwa karibu na vyombo vingine vya Udhibiti vya Serikali kama Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Mamlaka ya Chakula na Dawa Tanzania (TFDA), Mkemia Mkuu wa Serikali, Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), Tume ya Ushindani (FCC), Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Usafiri wa Nchi Kavu na Majini (SUMATRA). TBS kusaidia kitaalam (technical support) wazalishaji wadogo, wa kati na wakubwa wa ndani kufikia viwango vya ubora stahiki; TBS imekuwa ikishirikiana na Jeshi la Polisi na taasisi nyingine za Serikali kama TFDA, TRA, FCC, GCLA, EWURA katika kufanya ukaguzi wa kushitukiza masokoni ili kuhakikisha kuwa bidhaa hafifu, zilizo chini ya viwango na ambazo si salama kwa afya au matumizi ya mlaji zinaondolewa sokoni. Pili, Wizara imechukua hatua za kuijengea uwezo wa kupima sampuli kutoka 10,000 kwa mwaka

hadi kufikia 11,000 kwa mwaka, kuhakikisha kwamba maabara zote za Shirika zinapata vyeti vya umahiri (laboratory accreditation) na kuongeza idadi ya Watumishi. Tayari Maabara nne (4) za Ugezi, Kemia, Chakula na Nguo zimekwishapata vyeti vya umahiri. Tatu, kuingia Mikataba ya Ushirikiano na Taasisi kama TBS kwa upande wa Zanzibar na mchakato kama huo unaendelea kati ya Tanzania na China.

6.0 MAPATO NA MATUMIZI

6.1 Mapato

82. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2014/2015, Wizara imekusanya jumla ya Shilingi **7,263,159,533** (hadi Aprili, 2015) ikilinganishwa na makadirio ya Shilingi **5,204,719,000** sawa na asilimia 139.5. Makusanyo hayo yametokana na mauzo ya nyaraka za zabuni, ada za leseni, faini za leseni na malipo ya malimbikizo ya madeni.

6.2 Matumizi

83. ***Mheshimiwa Spika,*** Hadi kufikia Aprili, 2015, Wizara ilikuwa imekwishapokea jumla ya Shilingi **27,905,758,188** sawa na asilimia 85.86 kwa fedha za Matumizi ya Kawaida. Kati ya hizo, Shilingi. **6,865,963,673** ni fedha za Matumizi

Mengineyo (OC) na Shilingi **21,039,794,515** kwa ajili ya Mishahara. Aidha, jumla ya Shilingi **65,279,464,100** ya Miradi ya Maendeleo sawa na asilimia 83.05 zilipokelewa. Katika fedha za Miradi ya Maendeleo, Shilingi **64,600,000,000** ni fedha za ndani na Shilingi **679,464,100** ni fedha za nje. Fedha za mapato ziligawanywa kadri ilivyopangwa ambapo Wizara ilipata Shilingi **2,777,577,843** za kulipia Mishahara na Shilingi **4,199,663,175** za Matumizi mengineyo (OC) na fedha za Maendeleo Shilingi **1,479,464,100** wakati Taasisi zilipata Shilingi **2,666,300,498** fedha za Matumizi Mengineyo (OC) , Shilingi **20,720,875,807** za kulipia Mishahara na fedha za Maendeleo Shilingi **63,800,000,000.**

7.0 MAENDELEO YA RASILIMALI WATU

84. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara ina jumla ya watumishi 276, kati ya hao 107 ni wanawake na wanaume ni 169. Pia, kwa mwaka 2014/2015, Wizara imeajiri jumla ya watumishi 57 wa kada mbalimbali. Kati ya hao, Wachumi ni 16, Watakwimu 7, Afisa Biashara 14, Afisa Ugavi 2, Wachambuzi wa Mifumo ya Kompyuta 2, Katibu Mahsusi 4, Makarani Masjala 3, Afisa Utumishi 2, Afisa Tawala 3, Afisa Sheria 1, Afisa Habari 1, Mkaguzi wa Hesabu za Ndani 1 na Mhasibu 1. Aidha, Watumishi wote wa Wizara

wamesaini mikataba yao ya utendaji kazi (OPRAS) kwa wakati unaotakiwa. Aidha, Wizara imewathibitisha kazini watumishi 2 wa kada ya Makatibu Mahsusi, imepandisha vyeo watumishi 58 wa kada mbalimbali baada ya kuwa na utendaji mzuri wa kazi na kukidhi mahitaji ya Miundo yao ya kiutumishi. Aidha, vikao vya kiutendaji vya kila wiki, mwezi, na robo mwaka vimeendeshwa kama ilivyopangwa.

8.0 HUDUMA ZA SHERIA

85. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2014/2015, Wizara, kwa kushirikiana na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, imefanya mapitio na kurekebisha Sheria ya Stakabadhi za Ghala ya mwaka 2014 kwa lengo la kuboresha mfumo huo. Wakati huo huo marekebisho ya Sheria ya Ushindani yanaendelea ili kuboresha ushindani wa haki na utekelezaji. Muswada wake umekwishawasilishwa Bungeni kwa hatua zaidi. Aidha, Wizara imeshiriki katika majadiliano ya ununuzi wa Hisa 26 katika Kampuni ya *General Tyre (EA) Ltd.* Arusha.

9.0 MAMBO MTAMBUKA

9.1 Masuala ya Jinsia

86. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2014/2015, Wizara kwa kushirikiana na *UN Women,* ilichambua sera za Sekta ya Viwanda na Biashara (Analysis of Gender Oriented and Budget Responsive Policies) hususan Sera za Biashara na ya Viwanda) ili kujenga uwezo wa kitaasisi na kiutendaji wa Serikali katika kuandaa na kusimamia vyema sera na bajeti zinazozingatia mahitaji ya usawa wa kijinsia. Aidha, watumishi 80 walipata mafunzo ya mwitikio wa bajeti na masuala yanayoshabihiana na masuala ya jinsia na biashara. (Gender Responsive Budgeting and issues relating to Gender and Trade). Wizara imeongeza Uwezeshaji Biashara za Mipakani sanjali na kuwajengea uwezo wanawake 750 na wajasiriamali wengine wa mipakani wakati wa kuvusha bidhaa mipakani katika maeneo ya Dar-es-Salaam; Moshi; Arusha; Namanga; Mwanza; Mara; Musoma; Tarime; Sirari; Bukoba, Misenyi, Mutukula, Ngara, Rusumo na Kambanga.

9.2 Kupambana na Rushwa

87. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kupambana na kudhibiti rushwa kwa kuelimisha watumishi wake kwa kutoa mafunzo ya Sheria mbalimbali za kazi kama vile, Sheria ya Manunuzi ya Umma ya mwaka 2004,

Sheria ya Utumishi wa Umma Na. 8 ya mwaka 2002, Sheria ya Fedha pamoja na Sheria nyinginezo kwa lengo la kuweka misingi imara ya kisheria ili kupambana na rushwa. Aidha, Wizara imehuisha Mkataba wa Huduma kwa Mteja kwa lengo la kuweka wazi huduma inazozitoa na viwango vya huduma zake kufahamika kwa umma na hatimaye iweze kupata mrejesho wa kuboresha huduma zaidi.

9.3 Kupambana na UKIMWI / VVU

88. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imetekeleza program ya mapambano ya UKIMWI mahali pa kazi kwa kuhudumia watumishi wanaoishi na VVU na wenye UKIMWI kwa mujibu wa Waraka wa Serikali Na. 1 wa mwaka 2006 kuhusu huduma kwa wanaoishi na VVU na UKIMWI. Aidha, Wizara imeendelea kuhamasisha upimaji wa afya za wafanyakazi kwa hiari na kusambaza vifaa vya kuzuia maambukizi kama vile mipira ya kiume na kike kwa watumishi wake na taasisi zake.

10.0 MALENGO YA MWAKA 2015/2016

10.1 Sekta ya Viwanda

89. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2015/2016, utekelezaji katika Sekta ya Viwanda utazingatia malengo yafuatayo:-

(i) Kuendelea kutoa mafunzo ya kuongeza tija, ufanisi na ubora wa bidhaa kwa wenye viwanda kupitia Program za Kaizen na uimarishaji na uboreshaji viwanda (Industrial Upgrading and Modernization); na utafiti katika mifumo ya ubunifu (national systems of innovation survey) kwa kushirikiana na JICA na UNIDO sawia;

(ii) Kushiriki na kuhamasisha utekelezaji wa Mpango Kazi wa Sera ya Viwanda ya Jumuiya ya Afrika Mashariki na Mkakati na Mpango Kazi wa SADC;

(iii) Kufuatilia ufufuaji wa viwanda vilivyobinafsishwa ambavyo havifanyi kazi kikamilifu na kuanza ufufuaji wa Viwanda vya *General Tyre* na Urafiki;

(iv) Kukamilisha Sheria ya Kusimamia Biashara ya Chuma Chakavu na kuandaa kanuni zake;

(v) Kuendeleza utekelezaji wa Mkakati wa Kuendeleza Viwanda vya Ngozi na Bidhaa za Ngozi;

(vi) Kuendeleza utekelezaji wa Mkakati wa Kuendeleza Viwanda vya Nguo na Mavazi;

(vii) Kukamilisha Sensa ya Viwanda nchini kwa kushirikiana na Ofisi ya Taifa ya Takwimu;

(viii) Kurejea sheria zilizoanzisha taasisi za Utafiti wa Viwanda na Maendeleo (R & D Institutions) za CAMARTEC, TIRDO na TEMDO ili shughuli zake ziakisi na kuendana na mahitaji ya mfumo wa soko na pia taasisi husika kujitegemea; na

(ix) Kuandaa mfumo wa kuhawilisha teknolojia zinazobuniwa na taasisi za utafiti ili kuzalisha kibiashara (Commercialization of Prototype and Technology).

10.2 Sekta ya Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo

90. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2015/2016, Sekta ya Viwanda Vidogo na Biashara ina malengo yafuatayo:-

(i) Kuwezesha upatikanaji wa maeneo ya kufanyia kazi kwa wajasiriamali

wadogo na wa kati ikiwemo *Machinga* nchini;

(ii) Kuhamasisha uongezaji thamani wa mazao ya kilimo, mifugo, uvuvi na misitu na pia vito katika maeneo ya mijini na vijijini;

(iii) Kuwezesha wajasiriamali wadogo na wa kati kupata masoko ya bidhaa zao ndani na nje ya nchi;

(iv) Kufanya marejeo ya Sera ya Maendeleo ya Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo;

(v) Kuendelea kusimamamia Mradi wa Muunganisho Ujasiriamali Vijijini (MUVI) kwa muda ulioongezwa;

(vi) Kuimarisha na kupanua uwezeshaji kupitia huduma za kifedha na za kiufundi kwa njia za dhamana za Mikopo na Mikopo ya Moja kwa Moja yenye masharti nafuu kifedha kwa wajasiriamali wadogo na wakati;

(vii) Kuifanyia mageuzi makubwa SIDO ili iwe Mamlaka kamili ya uendelezaji Viwanda na Biashara Ndogo na za Kati; na

(viii) Kuanza ujenzi wa Mitaa ya Viwanda (Industrial Parks) kwa Mikoa Mipya ya Katavi na Njombe.

10.3 Sekta ya Biashara

91. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2015/2016, Wizara inatekeleza malengo katika Sekta ya Biashara yafuatayo:

(i) Kuendelea na majadiliano ya kibiashara kati ya Nchi na Nchi (*Bilateral*), Kikanda (*Regional*) na Kimataifa (*Multilateral*) kwa ajili ya kupanua wigo wa fursa za masoko yenye upendeleo wa ushuru wa forodha (duty free market access);

(ii) Kuendelea kuimarisha mfumo wa kukabiliana na Vikwazo vya Kibiashara Visivyo vya Kiushuru (*Non-Tariff Barriers*) na Uwezeshaji wa Biashara (*Trade Facilitation*) chini ya WTO kwa kushirikisha Kamati husika za Kitaifa za maeneo hayo;

(iii) Kuendelea kuimarisha Vituo vya Biashara vilivyopo London na Dubai ili kupanua Fursa za Masoko na Kuvutia Uwekezaji;

(iv) Kuratibu na kushiriki Majadiliano ya Kikanda kuhusu Biashara ya Huduma (*Trade in Services*) katika Jumuiya ya Maendeleo ya nchi za Kusini mwa Afrika (*SADC*), Eneo Huru la Utatu linalojumuisha Kanda

za *COMESA*, *EAC* na *SADC* (*Tripartite Free Trade Area*), Eneo Huru la Biashara la nchi za Afrika (*Continental Free Trade Area*), Biashara miongoni mwa nchi wanachama wa Afrika (*Boosting Intra African Trade*).

(v) Kuendelea na zoezi la kukamilisha Mapitio ya Sera ya Taifa ya Biashara ya mwaka 2003; na

(vi) Kuendelea kuhamasisha wadau kuhusu kuchangamkia fursa ya soko la AGOA na kutoa elimu na kuwahamasisha wananchi kuhusu fursa za masoko yaliyopo katika Jumuiya ya Ulaya (EPA).

10.4 Sekta ya Masoko

92. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2015/2016, Wizara katika Sekta ya Masoko ina malengo yafuatayo:-

(i) Kuendelea kuboresha Mazingira ya Biashara na Uwekezaji chini ya Mpango wa Matokeo Makubwa sasa – BRN;

(ii) Kuendeleza kutafuta masoko ya bidhaa za mazao katika nchi za Mashariki ya Kati na Asia na hususan

masoko ya nafaka, korosho zilizobanguliwa, nyama na bidhaa nyinginezo zilizoongezwa thamani;

(iii) Kuimarisha matumizi ya Mfumo wa Stakabadhi Ghalani na kuanzisha Mfumo wa Soko la Bidhaa (Commodity Exchange);

(iv) Kuandaa Sera ya Taifa ya Kumlinda Mlaji (National Consumer Protection Policy);

(v) Kuendeleza Miundombinu ya Masoko nchini;

(vi) Kuwezesha vikundi vya wakulima, wajasiriamali na wafanyabiashara kutangaza bidhaa na huduma za Tanzania katika masoko ya Ndani, Kikanda na Kimataifa kwa njia mbalimbali ikiwemo maonesho ya Kibiashara Kitaifa, Kikanda na Kimataifa;

(vii) Kuimarisha Mfumo wa Ukusanyaji Taarifa za Masoko;

(viii) Kuandaa Sera ya Taifa ya Viwango (National Standard Policy); na

(ix) Kuimarisha biashara za mipakani.

11.0 TAASISI CHINI YA WIZARA

93. ***Mheshimiwa Spika***, malengo ya Taasisi za Wizara ya Viwanda na Biashara kwa mwaka 2015/2016 ni kama ifuatayo:-

11.1. Kituo cha Zana za Kilimo na Teknolojia Vijijini (CAMARTEC)

(i) Kubuni na kutengeneza teknolojia za kuongeza tija na kupunguza harubu katika kilimo vijijini;

(ii) Kubuni na kutengeneza teknolojia za kuboresha usafiri na uchukuzi vijijini;

(iii) Kuendeleza utafiti na kuboresha mashine ya kuvuna, kupura mpunga (rice combine harvester); na

(iv) Kuendelea kurekebisha Sheria iliyoanzisha CAMARTEC ili kukidhi matakwa mapya.

11.2 Shirika la Uhandisi na Usanifu wa Mitambo (TEMDO)

(i) Kubuni na kuendeleza mtambo wa kusafisha maji taka (Water recycling system);

(ii) Kubuni na kuendeleza wa mtambo wa kuzalisha umeme utokanao na taka za mabaki ya mimea (Electricity generation from biomass);

(iii) Kuendeleza na kuhamasisha utengenezaji kibiashara wa mitambo ya kuteketeza taka za hospitali kwa ajili ya matumizi katika Sekta ya Afya nchini. Vilevile, taasisi itabuni na kuendeleza kiteketezi maalum (sanitary pad burner) kwa ajili ya matumizi katika shule na vyuo vyenye wanawake nchini;

(iv) Kuendeleza mtambo wa kuzalisha nishati itokanayo na mabaki ya mimea (Biomass briquetting) kupitia wajasiriamali watengenezaji;

(v) Kuendeleza mtambo wa kusindika na kusafisha mafuta ya kula kupitia wajasiriamali watengenezaji;

(vi) Kutangaza shughuli za taasisi kupitia vyombo vya habari na kushiriki kwenye maonesho ya kibiashara ili kutangaza chasili (prototypes) zilizo tengenezwa;

(vii) Kubuni na kuendeleza bidhaa maalum za kuzuia na kutunza joto (refractory products) kwa kutumia malighafi inayopatikana nchini; na

(viii) Kubuni na kuendeleza mtambo wa kisasa (hybrid system) unao zalisha umeme utokanao na jua pamoja na upepo.

11.3 Taasisi ya Utafiti na Maendeleo ya Viwanda (TIRDO)

(i) Kufanya utafiti na kutoa mafunzo ya Sekta ya Ngozi jinsi ya kuhifadhi na kurejesha taka za ngozi ili kutengeneza bidhaa kama 'Leather boards' na hivyo kulinda mazingira;

(ii) Kufanya utafiti na kutoa mafunzo ya utunzaji siri kupitia Mitandao (Cyber Security) katika Viwanda, Taasisi za Serikali na Wakala wa

Serikali kulingana na (Waraka wa Katibu Mkuu Kiongozi Na 1 wa mwaka 2011);

(iii) Kutekeleza Mpango wa Matumizi Bora ya Rasilimali za TIRDO ikiwemo ardhi yake baada ya Mpango husika kupitishwa na Serikali;

(iv) Kuboresha Maabara ya Mazingira na ya Vifaa vya Kihandisi ili ziweze kufikia viwango vya kimataifa (Accreditation) ili kutoa huduma bora kwa wazalishaji viwandani;

(v) Kuendelea kutekeleza Mfumo wa Ufuatiliaji wa Mazao (Agricultural Products Traceability) kwa kutumia TEHAMA na pia kuisaidia kiushauri kampuni ya GS1 (TZ) kama mshauri wa kiufundi;

(vi) Kukamilisha marekebisho ya Sheria ya Bunge Na. 5 ya mwaka 1979 iliyoanzisha TIRDO;

(vii) Kutoa ushauri wa kitaalam na kiufundi kwenye maeneo yote yanayohusu kilimo na sekta zinazoibukia za mafuta na gesi; na

(viii) Kuendelea kutoa huduma za kitaalam viwandani ili kuongeza uzalishaji wa bidhaa bora bila kuchafua mazingira au kutumia nishati hovyo.

11.4 Shirika la Viwango Tanzania (TBS)

(i) Kuendeleza utekelezaji wa utaratibu wa kupima ubora wa bidhaa zote mahali zinapotoka kabla ya kuingia nchini (*Preshipment Verification of Conformity to Standards – PVoC*);

(ii) Kuendelea kushirikiana kwa karibu na vyombo vingine vya Serikali kuhakikisha kuwa bidhaa zinazoingia nchini ni zenye ubora unaokubalika;

(iii) Kuongeza idadi ya Leseni za Ubora wa Bidhaa kutoka 100 mwaka 2014/2015 hadi 120 mwaka 2015/2016;

(iv) Kuongezeka idadi ya upimaji sampuli kutoka 11,000 katika mwaka 2014/2015 hadi 12,000 mwaka 2015/16;

(v) Kutayarisha viwango vya kitaifa vinavyofikia 250 vikiwemo viwango vya Sekta ya Huduma katika mwaka 2015/2016;

(vi) Kuziboresha maabara zote za Shirika ili kufikia hadhi ya umahiri na kutambulika Kimataifa (*laboratory accreditation*);

(vii) Kuendelea kutoa mafunzo kwa wajasiriamali nchini kote kuhusu viwango vya udhibiti wa ubora wa bidhaa na kuongeza vyeti vya ubora wa bidhaa zinazoagizwa kutoka nje ya nchi; na

(viii) Kuendelea kuimarisha utaratibu wa kukagua ubora wa bidhaa ukiwemo ukaguzi wa magari kabla ya kuingia nchini.

11.5 Baraza la Ushindani (FCT)

(i) Kusikiliza kesi za rufaa zinatokana na mchakato wa udhibiti na ushindani wa biashara kwenye soko;

(ii) Kujenga uwezo zaidi wa ujuzi na weledi katika kushughulikia masuala ya ushindani na Wajumbe wa Baraza;

(iii) Kuendelea kutoa elimu kwa umma juu ya kazi za Baraza na umuhimu wake katika uchumi; na

(iv) Kuimarisha upatikanaji wa rasilimali fedha ili kuongeza ufanisi wa Sekretarieti na Baraza.

11.6 Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA)

(i) Kuendelea kuweka na kuboresha Mfumo wa Usajili wa Majina ya Biashara (Business Names Registration) na Usajili wa Makampuni (Company Registrar) na huduma nyingine za BRELA kwa njia ya Mtandao (On line registration systems);

(ii) Kurekebisha Sheria za Wakala ili ziweze kwenda na wakati;

(iii) Kuboresha mifumo ya uwekaji na utunzaji wa masijala tano za

kisheria zinazosimamiwa na Wakala ili ziweze kushabihiana na mfumo wa TEHAMA unaowekwa sasa ili hatimaye kurahisisha utoaji huduma;

(iv) Kuendelea kuelimisha umma kuhusu shughuli za Wakala na umuhimu wa kusajili biashara;

(v) Kuendeleza watumishi na kuweka mazingira mazuri ya utendaji kazi ili kuongeza tija na uwajibikaji;

(vi) Kuendeleza mahusiano na mashirika ya Kikanda na Kimataifa ambayo Tanzania ni mwanachama;

(vii) Kuanza kwa ujenzi wa Jengo la BRELA kwa ajili ya Ofisi na Masijala;

(viii) Kuendeleza na kuimarisha mahusiano mazuri na ushirikiano na taasisi mbalimbali za ndani ya nchi na pia Sekta Binafsi katika kufanikisha shughuli za Wakala; na

(ix) Kutafuta rasilimali fedha kwa ajili ya kugharamia shughuli za maendeleo za Wakala ikiwemo ujenzi wa jengo la Wakala.

11.7 Tume ya Ushindani (FCC)

(i) Kulinda na kuendeleza ushindani katika soko;

(ii) Kumlinda mlaji; na

(iii) Kupambana na kudhibiti bidhaa bandia na kutoa elimu ya bidhaa bandia kwa mlaji (Consumer and Counterfeit Education).

11.8 Baraza la Taifa la Utetezi wa Mlaji (NCAC)

(i) Kuandaa Sera ya Taifa ya Kumlinda Mlaji na Mkakati wake;

(ii) Kuendelea kukamilisha ikama, Kanuni za Utumishi na za fedha za Baraza;

(iii) Kulinda maslahi ya mlaji kwa kupeleka maoni yake kwenye Tume ya Ushindani, Mamlaka za Udhibiti na Serikali kwa ujumla;

(iv) Kuendelea kupokea na kusambaza taarifa na maoni yenye maslahi kwa mlaji; na

(v) Kuanzisha Kamati za Mlaji za Mikoa na za Kisekta zitakazotoa ushauri kwa Wizara, wenye viwanda na jumuiya nyingine za walaji katika mambo yenye maslahi kwa mlaji.

11.9 Bodi ya Leseni za Maghala (TWLB)

(i) Kujaza nafasi zilizo wazi katika Bodi;

(ii) Kujenga uwezo wa Watendaji wa Bodi kwa ajili ya kuongeza weledi na ufanisi wa utendaji;

(iii) Kutafuta na kuboresha vyanzo vya mapato vya Bodi;

(iv) Kujenga mahusiano ya karibu zaidi na wadau wakuu, yaani Watunza Mali, Wanunuzi, Waendesha Maghala na Taasisi za fedha kwa kuboresha mfumo wa utoaji leseni, kutoa elimu ikiwemo kuendesha makongamano ya wadau; na kuhamasisha huduma za kibenki wa wakulima vijijini;

(v) Kuhamasisha na kuhakikisha uwepo wa uwazi, uwajibikaji, na kuzuia mazingira ya utoaji na upokeaji wa rushwa katika Baraza;

(vi) Kufungua Ofisi za Kanda kwa ajili ya uendeshaji Mfumo wa Stakabadhi Ghalani na Soko la Bidhaa;

(vii) Kukamilisha maboresho ya Sheria Na. 10 ya mwaka 2005 kwa kuandaa Kanuni za Sheria husika; na

(viii) Kuhamasisha uanzishwaji na matumizi ya *Electronic Warehouse Receipt System* sambamba na uanzishwaji wa

Soko la Bidhaa nchini (Tanzania Commodity Exchange).

11.10 Chama cha Hakimiliki Tanzania (COSOTA)

(i) Kufungua Ofisi ya Kanda ya Hakimiliki mjini Arusha, kwa ajili ya Kanda ya Kaskazini na mjini Dodoma kwa ajili ya Kanda ya Kati na Magharibi;

(ii) Kukamilisha marekebisho ya Sheria ya Hakimiliki na Hakishiriki ya mwaka 1999;

(iii) Kuanza utaratibu wa kusambaza Stika (Hakigram) kwa wasambazaji wote wa kazi za muziki na filamu;

(iv) Kuhamasisha wanunuzi wa CD, Kanda za Muziki na filamu kununua Kanda na CD zenye *Hakigram*; na

(v) Kuingia mkataba na makampuni binafsi kwa lengo la kukusanya mirabaha na

kufanya operesheni dhidi ya kazi bandia.

11.11 Wakala wa Vipimo (WMA)

(i) Kuimarisha usimamizi wa matumizi ya vipimo vilivyo sahihi nchini kupitia uimarishwaji wa uhakiki na ukaguzi wa vipimo hivyo ili kumlinda mlaji na mfanyabiashara;

(ii) Kuongeza mbinu za utoaji wa elimu ya matumizi ya vipimo sahihi ili kuongeza uelewa wa matumizi yake na ufungashaji wa bidhaa;

(iii) Kuimarisha Kitengo cha Vipimo Bandarini (WMA Ports Unit);

(iv) Kukamilisha utafiti na uchambuzi wa mfumo wa vipimo vya usambazaji wa gesi asilia (Natural Gas);

(v) Kuendelea na zoezi la kuandaa kanuni mpya ya ufungashaji wa gesi kwenye mitungi;

(vi) Kuendelea na kazi ya ujenzi wa kituo cha kupimia magari yanayosafirisha mafuta katika eneo la Misugusugu - Pwani, Kituo cha Mwanza na Iringa;

(vii) Kukamilisha utungaji wa Sheria mpya ya Vipimo (Legal Metrology Act); na

(viii) Kuendelea kuboresha mazingira ya kazi kwa kuongeza vitendea kazi.

11.12 Shirika la Maendeleo la Taifa (NDC)

(i) Kusimamia utekelezaji wa miradi ya Makaa ya Mawe ya Mchuchuma na Ketewaka, na Chuma cha Liganga - Njombe;

(ii) Kusimamia utekelezaji wa Mradi wa Kuzalisha Chuma Ghafi (Njombe);

(iii) Kukamilisha ujenzi na kuzindua uzalishaji katika Kiwanda cha Kuzalisha Viuadudu, (Biolarvicides) kwa ajili ya kuua viluwiluwi kwenye mazalia ya mbu wa malaria Mkoani (Pwani) Kibaha;

(iv) Kuendelea na uchimbaji wa Makaa ya Mawe Ngaka Kusini na kuanzisha ujenzi wa Kituo cha Kufua Umeme (Ruvuma);

(v) Kujenga mitambo ya kuzalisha umeme kwa kutumia nguvu za upepo Singida;

(vi) Kufufua Kiwanda cha Kutengeneza Matairi cha *General Tyre,* Arusha;

(vii) Kusimamia na kutekeleza Kiwanda cha Kuzalisha Magadi Soda Engaruka Arusha;

(viii) Kufufua Kiwanda cha KMTC, Kilimanjaro;

(ix) Kuendeleza mashamba ya mpira ya Kalunga (Morogoro), Kihuhwi

(Tanga) na kuanzisha mashamba mengine;

(x) Kutekeleza mradi wa Kilimo cha Michikichi na Kiwanda cha Kuzalisha Mafuta ya Mawese (Kisarawe, Pwani);

(xi) Kujenga Maeneo ya Viwanda (Industrial Parks) sehemu za TAMCO (Kibaha), KMTC (Kilimanjaro), Kange (Tanga) n.k.;

(xii) Kuratibu uendelezaji wa Kanda za Maendeleo za Mtwara, Tanga, Kati na Uhuru; na

(xiii) Kujenga uwezo wa wananchi wa maeneo ya Miradi ya Kimkakati yaliyoanishwa katika Dondoo (i) – (xii) hapo juu ili wafaidike na miradi inayotekelezwa na NDC.

11.13. Mamlaka ya Maeneo Maalum ya Kuzalisha Bidhaa za Kuuza Nje (EPZA)

(i) Kuendelea na utekelezaji wa Mkakati Unganishi wa

Uendelezaji Viwanda Nchini kwa kuhamasisha uwekezaji katika uongezaji thamani mazao ya kilimo, mifugo, uvuvi, misitu na madini;

(ii) Kuendelea kuhamasisha na kusimamia uendelezaji na uwekezaji katika maeneo ya EPZ na SEZ ikiwemo ujenzi wa *Logistics Centre* za Kurasini na Kigoma, Bandari na Industrial Park Bagamoyo;

(iii) Kunadi miradi/maeneo ya SEZ za Bagamoyo, Bunda na Mererani kwa wawekezaji

11.14 Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE)

(i) Kuandaa mitaala mipya ya taaluma ya usimamizi wa nishati ya mafuta na gesi, ujasiriamali na elimu ya biashara katika ngazi ya shahada na shahada ya umahiri (Masters Degree);

(ii) Kuimarisha uwezo wa wakufunzi *(capacity building)*

katika mafunzo ya muda mrefu katika ngazi ya shahada za umahiri na uzamivu;

(iii) Kuanza ujenzi wa Kampasi ya Mwanza katika kiwanja cha Kiseke kwa kuzingatia *master plan*;

(iv) Kuboresha miundombinu ya Kampasi ya Dar es Salaam na Dodoma; na

(v) Kukamilisha upatikanaji wa eneo la ujenzi wa Kampasi ya Mbeya na kuandaa *master plan* yake.

11.15 Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo (SIDO)

(i) Kuratibu na kuwezesha uanzishwaji wa Kongano za Viwanda (Industrial Clusters) wa uzalishaji bidhaa mbalimbali;

(ii) Kuendelea na uanzishaji wa mitaa ya viwanda katika Mikoa mpya;

(iii) Kuwezesha uboreshaji wa vyumba vya kutolea mafunzo katika ofisi za mikoa;

(iv) Kukiongezea uwezo Kituo cha Maendeleo ya Teknolojia Shinyanga kufikia hadhi ya kuwa kituo kamili;

(v) Kuimarisha mfumo wa TEHAMA wa SIDO ili pamoja na mambo mengi kuweza kufuatilia utendaji;

(vi) Kujenga majengo matano (5) ya Ofisi za SIDO katika mikoa ya Morogoro, Katavi, Njombe, Simiyu na Geita; na

(vii) Kujenga uwezo wa Vituo vya Maendeleo ya Teknolojia vya SIDO kuzalisha mashine ndogo za uongezaji thamani mazao ya kilimo hasa vijijini;

(viii) Kujenga uelewa wa wajasiriamali mahitaji ya ufikiwaji wa ubora na viwango kulingana na matakwa ya TFDA na TBS;

(ix) Kutoa elimu ya ujasiriamali, usimamizi wa biashara na usindikaji wa vyakula;

(x) Kuwawezesha wazalishaji wadogo kupata taarifa za masoko ya bidhaa na huduma zao kwa kuwawekea miundombinu ya kupokea na kusambazia habari za kibiashara, kutengeneza sehemu za kuoneshea bidhaa za wazalishaji wadogo;

(xi) Kuendelea kuchangia katika gharama za utekelezaji wa mradi wa Kuendeleza Ujasiriamali Vijijini (MUVI); na

(xii) Kuuongezea uwezo wa kifedha Mfuko wa NEDF, kutoa huduma za kifedha ikiwa ni pamoja na ushauri na mikopo pale itakapojidhihirisha kuhitaji.

11.16 Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (TANTRADE)

(i) Kuwajengea uwezo wajasiriamali ili waweze kuzijua fursa na jinsi

ya kuzimudu changamoto za masoko ya ndani na nje;.

(ii) Kuwapa ujuzi wafanyabiashara wanawake wakiwemo wa sekta isiyo rasmi jinsi ya kuendesha shughuli zao katika mipaka ya Jumuiya ya Afrika ya Mashariki (Trade facilitation for Women Informal Cross-Border Traders in the East Africa Community), ambayo ni mipaka ya Manyovu, Kabanga, Lusumo, Mtukula, Sirari, Namanga, Horohoro, Horiri na Tarakea;

(iii) Kutafuta masoko ya nje kwa kuratibu Maonesho ya Biashara ya Kimataifa ya nchi za nje;

(iv) Kuwaunganisha wafanyabiashara wetu na wadau wafanyabiashara wengine wa ndani na nje ya nchi, na pia kuwapa uelewa wa mwenendo wa bei za bidhaa kitaifa na kimataifa;

(v) Kuendeleza soko la ndani kwa kusisimua maendeleo ya biashara;

(vi) Kutoa taarifa za kibiashara kwa wafanyabiashara wa Tanzania;

(vii) Kushiriki katika kuboresha mfumo na sera za biashara; na

(viii) Kuimarisha Ofisi ya Tantrade Zanzibar.

11.17 Kituo cha Biashara cha Tanzania Dubai- (TTC-DUBAI)

(i) Kuongeza mauzo ya matunda na mbogamboga hususan baada ya kuongezeka kwa uwezo wa kusafirisha mzigo kwa ndege na kupungua kwa bei ya *freight* kwenda UAE na kuisaidia TAHA katika uhamasishaji na uwekezaji kwenye *Pack House* Nyanda za Juu;

(ii) Kuandaa misafara, kwa kushirikiana na *Dubai Multi Commodity Center* na *Dubai Exports*, ya wanunuzi wa madini na vito kutembelea Maonesho ya Vito ya Wizara ya Nishati na

Madini ya mwezi Aprili na Novemba, 2015 kila mwaka mjini Arusha; na

(iii) Kushirikiana na *Jebel Ali Free Zone Authority* na *Dubai Exports,* kuandaa ziara za wawekezaji kujionea fursa za kuwekeza kwenye Maeneo Maalum ya Uwekezaji huru *"Special Economic Zone"* ya Bagamoyo.

11.18 Kituo cha Biashara cha Tanzania London (TTC-LONDON)

(i) Kuiwakilisha nchi katika Maonesho ya Utalii nchini Uingereza na Ulaya kwa ujumla kwa lengo la kukuza na kuitangaza vyema nchi kwenye Sekta ya Utalii;

(ii) Kuitumia Mikutano na Matamasha makubwa ya uwekezaji Uingereza na Ulaya, mathalan *Africa Ireland Economic Forum* mwezi Oktoba, 2015 mjini Dublin kutangaza fursa za uwekezaji zilizoko nchini;

(iii) Kuandaa mikutano midogo ijulikanayo kama *Investment Breakfasts* kwa wawekezaji kubadilishana mawazo, uzoefu na kujibu hoja mbalimbali ili kuwapa moyo wawekezaji wenye nia ya kuwekeza nchini Tanzania; na

(iv) Kukuza Diplomasia ya Uchumi, kwa kufuatilia shughuli za Mashirika ya Kimataifa yaliyoko London ambayo Tanzania ni mwanachama.

12.0 MASUALA MTAMBUKA

94. ***Mheshimiwa Spika,*** mambo mtambuka yatakayotekelezwa na Wizara katika mwaka 2015/2016 ni yafuatayo:

12.1 Maendeleo ya Rasilimali Watu

(i) Kuajiri watumishi kumi na tano (15) wa kada mbali mbali;

(ii) Kuthibitisha kazini watumishi hamsini na saba (57) na kuwathibitisha katika vyeo watumishi hamsini na nane (58);

(iii) Kupandisha vyeo watumishi thelathini na moja (31) baada ya kupimwa utendaji kazi wao;

(iv) Kujenga uwezo kwa watumishi wake kwa kuwapeleka mafunzo ya muda mrefu na mfupi ndani na nje ya nchi;

(v) Kutoa huduma stahiki kwa viongozi na watumishi wa Wizara kwa kuzingatia Taratibu, Miongozo, Kanuni na Sheria za Utumishi wa Umma pamoja na kuratibu na kusimamia masuala yote ya uendeshaji wa shughuli za Wizara; na

(vi) Kujenga afya za watumishi kupitia programu mbalimbali za michezo na pia kujenga ushirikiano na kufahamiana

12.2 Kudhibiti Rushwa

(i) Kuratibu utekelezaji wa Mkakati wa Kupambana na Rushwa;

(ii) Kutoa mafunzo kwa watumishi wake na kwa kupitia Kamati ya Maadili kuhakikisha kila Idara na Vitengo inajiwekea mikakati yao juu ya rushwa; na

(iii) Kusimamia utekelezaji wa Mkataba wa Huduma kwa Mteja pamoja na kutoa elimu ya huduma kwa mteja kwa watumishi 50.

12.3 Janga la UKIMWI na Magonjwa Sugu Yasiyoambukizwa

(i) Kuendelea kutekeleza Mwongozo wa mwaka 2014 unaohusu masuala ya UKIMWI na Magonjwa sugu yasiyoambukizwa mahali pa kazi; na

(ii) Kuhuisha Kamati ya Kushughulikia Masuala ya UKIMWI sehemu ya kazi kwa mujibu wa mwongozo na kutoa mafunzo kwa watumishi.

12.4 Masuala ya Jinsia

(i) Kuendelea kutoa elimu ya dhana ya Jinsia kwa wadau wa sekta hususan maafisa biashara mikoani na maafisa wanaoshughlikia masaula ya wanawake mipakani; na

(ii) Kuendelea kutatua kero za wanawake wafanyabiashara hasa mitaji kwa kuanzisha Dawati la Kushughulikia Masuala ya Jinsia kwenye mipaka ya Tanzania na nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki.

13.0 MAOMBI YA FEDHA KWA MWAKA 2015/2016

13.1 Mapato ya Serikali

95. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2015/2016, Wizara inatarajia kukusanya Shilingi **10,000,002,000** ikilinganishwa na Shilingi **5,204,719,000** kwa mwaka 2014/2015 kutokana na ada za leseni za biashara, nyaraka za zabuni, faini kwa kukiuka sheria ya leseni na makusanyo mengineyo.

13.2 Maombi ya Fedha

96. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2015/2016, Wizara ya Viwanda na Biashara inaomba kutengewa jumla ya shilingi **116,496,769,000** ili kutekeleza majukumu ya kuindeleza Sekta ya Viwanda na Biashara. Kati ya fedha hizo, Shilingi **53,697,588,000,** sawa

na asilimia 46 ya bajeti ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Shilingi **62,799,181,000,** sawa na asilimia 54 ya bajeti ni kwa ajili ya Matumizi ya Maendeleo.

97. ***Mheshimiwa Spika***, katika bajeti ya Shilingi **62,799,181,000** iliyotengwa kwa ajili ya Matumizi ya Maendeleo, Shilingi **54,000,000,000** ni fedha za ndani na Shilingi **8,799,181,000** ni fedha za nje zinazotokana na Washirika wa Maendeleo.

13.2.1 Fedha za Ndani

98. ***Mheshimiwa Spika***, Miradi itakayotekelezwa kwa fedha za ndani ni pamoja na *Tanzania Mini Tiger Plan* 2020 Shilingi **22,300,000,000** zimetengwa kulipia fidia eneo la Bagamoyo SEZ; Shilingi **3,796,400,000** kulipia fidia eneo la *Tanzania China Logistics Center* - Kurasini; *Mchuchuma Coal* Shilingi **5,000,000,000** zitatumika kuendeleza utekelezaji wa miradi ya Kasi Mpya na Makaa ya Mawe ya Mchuchuma; Shilingi **5,000,000,000** zitatumika kutekeleza Mradi wa Chuma cha Liganga na Shilingi **3,750,000,000** zimetengwa kwa ajili ya ASDP kuchangia katika utekelezaji wa miradi ya Sekta ya Kilimo inayojumuisha uanzishaji wa Soko la Mazao na Bidhaa. Aidha, NDC - *Malaria Project* imetengewa Shilingi

1,190,000,000 ili kukamilisha ujenzi wa Kiwanda cha Kuzalisha Viuadudu (biolarvicides) vya Kuua Viluwiluwi wa Mbu Waenezao Malaria katika eneo la TAMCO-Kibaha kwa kujenga bwawa la maji taka (oxidation pond) na kuanza uzalishaji, Shilingi **7,413,600,000** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo iliyopo kwenye Mashirika na Taasisi zilizo chini ya Wizara, Shilingi **10,000,000** kwa ajili ya kusaidia Mradi wa *Gender Mainstreaming in Trade Sector and Micro and Small Enterprise Development Strategy,* Shilingi **800,000,000** kwa ajili ya Mradi wa *Promoting Investment in the Soda Ash Project at lake Natron and Engaruka Basin,* Shilingi **1,000,000,000** kwa ajili ya mradi wa *SMES Industrial Infrastructure Expan. & Capacity Build,* Shilingi **680,000,000** kwa ajili ya utekelezaji wa Mradi wa BEST (Continue to improve business environment and investment climate (BRN), Sh **200,000,000** kwa ajili ya *Rural Micro, Small And Medium Enterprises Support Programme (MUVI),* Shilingi **600,000,000** kwa ajili ya Singida *Wind Power Project-Harnessing Renewable and Sustainable Energy Supplies in Tanzania*, Shilingi **10,000,000** kwa ajili ya UNIDO - *Integrated Industrial Development Programmes,* Shilingi **1,800,000,000** kwa ajili ya Kununua Hisa Asilimia 26 (26%) za *AG Continental* katika Kampuni ya *General Tyre East Africa (GTEA)* ili

Serikali iweze kumiliki Kiwanda kwa 100% (Revival of General Tyre and Rubber Plantations), Shilingi **100,000,000** kwa ajili ya *Kaizen Programme* yenye lengo la Kuendelea kutoa mafunzo ya kuongeza tija, ufanisi pamoja na ubora wa bidhaa kwa wenye viwanda kupitia program ya *Kaizen* kwa kushirikiana na Shirika la Misaada la Japan (JICA), Shilingi **250,000,000** kwa ajili ya Kuimarisha uwezo wa Bodi ya leseni za Maghala Tanzania ili kutoa huduma bora katika utekelezaji wa Mfumo wa Stakabadhi za Maghala nchini na Shilingi **100,000,000** kwa ajili ya *Support for Trade Mainstreaming.*

13.2.2 Fedha za Nje

99. ***Mheshimiwa Spika***, bajeti ya Shilingi 8,799,181,000 ya fedha za Maendeleo za Nje zitatumika katika kutekeleza miradi ya maeneo mbalimbali kama ifuatayo:

(a) *Rural Micro, Small and Medium Enterprises Support Programme (MUVI)* umetengewa Shilingi 6,172,639,000;

(b) *Support for Trade Mainstreaming* umetengewa Shilingi 1,384,000,000;

(c) *Strengthening TWLB Capacity for efficiency in Warehouse Receipt System (WRS) service provision in Tanzania* umetengewa Shilingi 192,542,000; na

(d) *Implementation of BEST Programme* umetengewa Shilingi 1,050,000,000.

14.0 HITIMISHO

100. ***Mheshimiwa Spika***, naomba nichukua fursa hii kuwashukuru tena Watanzania wote kwa kutuunga mkono katika jitihada zetu za kuendeleza Sekta ya Viwanda na Biashara katika kipindi chote cha Awamu ya Nne. Katika kipindi hicho tumejitahidi kujenga na kuimarisha misingi thabiti ya kujenga uchumi unaoongozwa na viwanda kama ilivyobainishwa katika DIRA 2025. Ni jukumu kubwa na nyeti ambalo linapaswa kuendelea kuungwa mkono na wapenda maendeleo wote na hasa Watanzania na wazalendo wote. Ushindani katika maendeleo ni mkubwa sana, na ni katika kujijengea uwezo wa kiushindani katika soko, ndiko matumaini ya kesho ya Taifa yaliko. Hivyo, kila Mtanzania hana budi kujituma, kubadilisha mtizamo na kuwa mstari wa mbele kulinda na kutetea jitihada na

kuendeleza Viwanda na Biashara yetu kwa maslahi ya nchi yetu. Jana ni historia, lakini Tanzania yetu ya leo na kesho ni dira iliyoko mikono mwetu. Hutuba hii pia inapatikana katika tovuti ya Wizara (www.mit.go.tz)

101. ***Mheshimiwa Spika,*** naomba kutoa hoja.

VIAMBATISHO

JEDWALI NA. 1: MASHIRIKA NA MAJUKUMU YAKE MUHIMU

NA	JINA LA TAASISI	MAJUKUMU YAKE
1	Shirika la Utafiti na Maendeleo ya Viwanda Tanzania (TIRDO)	Kufanya utafiti na kutoa ushauri wa kiufundi kwa viwanda. Kuhamasisha matumizi ya teknolojia yenye kutumia malighafi za Tanzania viwandani na kubuni/kuunda spea za viwandani kwa kutumia malighafi za nchini.
2	Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo (SIDO)	Kuhamasisha maendeleo ya Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo nchini.
3	Kituo cha Zana za Kilimo na Ufundi Vijijini (CAMARTEC)	Kuendeleza na kusambaza teknolojia zilizoboresha endelevu kwa ajili ya kilimo na maendeleo vijijini. Kuboresha maisha ya waishio vijijini kupitia uendelezaji na matumizi ya teknolojia sahihi katika kilimo cha kutumia

NA	JINA LA TAASISI	MAJUKUMU YAKE
		mitambo ya kisasa, usambazaji wa maji, vifaa vya ujenzi, usafiri vijijini na nishati.
4	Shirika la Uhandisi na Usanifu wa Mitambo (TEMDO)	Kuhamasisha ubunifu/uundaji wa teknolojia za viwanda, maendeleo ya teknolojia na kuhamasisha kampuni za nchini kushindania katika utaoji wa huduma bora za kiufundi.
5	Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (TANTRADE)	Kusimamia na kuratibu Biashara ya Ndani na Nje.
6	Shirika la Maendeleo la Taifa (NDC)	Kuchochea maendeleo ya viwanda mama nchini
7	Bodi ya Leseni za Maghala Tanzania (TWLB)	Kuendeleza masoko ya mazao ya wakulima kwa kuondoa vikwazo vinavyokwamisha uzalishaji na masoko.
8	Shirika la Viwango Tanzania (TBS)	Uandaaji na utekelezaji wa viwango vya Tanzania, ikiwa ni pamoja utoaji wa vyeti vya alama ya ubora,

NA	JINA LA TAASISI	MAJUKUMU YAKE
		uhakiki wa ubora, upimaji wa vifaa vinavyotumika kupima ubora wa bidhaa viwandani yaani ugezi, kutoa elimu katika uwekaji na usimamizi wa viwango.
9	Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE)	Kutoa mafunzo kwa njia ya vitendo yaliyobobea katika elimu ya biashara.
10	Kituo cha Biashara - London (LTC)	Kutangaza maslahi ya kiuchumi na kuanzisha mahusiano ya kimkakati ya kibiashara na Uingereza na nchi nyingine za Jumuiya ya Ulaya na duniani.
11	Kituo cha Biashara Dubai (DTC)	Kuhamasisha uwekezaji, utalii na biashara nchini katika eneo la Mashariki ya Kati.
12	Tume ya Ushindani (FCC)	Kuhakikisha ushindani wa haki unakuwepo ili kumlinda mlaji kutokana na matumizi mabaya ya nguvu ya soko
13	Baraza la Ushindani Tanzania (FCT)	Kusikiliza na kuamua rufaa kutoka Tume ya Ushindani na Mamlaka za

NA	JINA LA TAASISI	MAJUKUMU YAKE
		Udhibiti za EWURA, SUMATRA, TCAA na TCRA .
14	Baraza la Taifa la Kulinda Mlaji (NCAC)	Kulinda na kumtetea mlaji nchini.
15	Mamlaka ya Maeneo Maalum ya Uwekezaji kwa Mauzo ya Nje (EPZA)	Kuratibu, kuhamasisha na kuvutia uwekezaji katika maeneo huru ya uwekezaji kwa ajili ya mauzo nje.
16	Wakala wa Usajili Biashara na Leseni za Viwanda (BRELA),	Usajili wa Makampuni, Majina ya Biashara, Alama za Biashara na Huduma, kutoa Hataza, kutoa Leseni za Viwanda na kuratibu masuala ya Miliki Ubunifu.
17	Wakala wa Mizani na Vipimo (WMA),	Kulinda walaji katika masuala ya vipimo na mizani.
18	Chama cha Hakimiliki Tanzania (COSOTA),	Kuhamasisha, kutetea, kukuza na kulinda maslahi ya waandaji wa kazi zinazolindwa na Sheria ya Hakimiliki, wachapishaji, wanamuziki, waandishi na kukusanya na kugawa mirahaba.

Jedwali Na. 2	**Vigezo vya Ufanisi katika Sekta ya Viwanda**				
Mwaka	**Mchango katika Pato la Taifa % (Bei za 2007)**	**Ukuaji wa Sekta (Bei za 2007)**	**Mchango katika Mauzo ya nje %**	**Mchango katika Mauzo nje yasiyo Asilia (%)**	**Ongezeko la mauzo nje ya bidhaa za viwanda(%)**
2005	6.59		9.31	11.81	
2006	6.83	8.4%	11.23	13.81	25.4%
2007	7.02	11.5%	15.28	18.14	57.9%
2008	7.41	11.4%	20.73	28.48	139.9%
2009	7.36	4.7%	15.36	21.35	-31.7%
2010	7.54	8.9%	22.29	30.34	90.3%
2011	7.47	6.9%	16.90	22.99	-10.6%
2012	7.40	4.1%	17.61	24.91	20.4%
2013	7.35	6.5%	20.39	28.95	3.3%
2014	7.34	6.8%	23.31	32.66	15.6%

Chanzo: Wizara ya Fedha

Jedwali Na. 3 Uzalishaji wa Baadhi ya Bidhaa Viwandani

Aina ya Bidhaa	Kipimo	2007	2008	2009	2010	2011	2012	2013	2014	2013/14 Badiliko(%)
Biskuti & tambi	Tani	11273	15435	15200	7435	12053	16006	17440	18225	4.5%
Unga wa ngano	Tani	406336	287925	368885	444242	439926	443731	516778	529797	2.5%
Konyagi	000 Lita	5622	4049	10201	11186	15432	16774	20680	31963	54.6%
Bia	000 Lita	310194	291178	284906	242689	323393	338650	374238	379913	1.5%
Chibuku	000 Lita	10320	10235	16141	21037	23474	22028	19935	20301	1.8%
Sigara	Milioni	5821	6101	5831	6181	6630	7558	7710	8028	4.1%
Nguo	000 M^2	139000	140531	91501	103177	101820	83592	97522	119458	22.5%
Kamba za katani	Tani	7012	7783	7913	6872	6976	7754	7542	7871	4.4%
Nyavu za uvuvi	Tani		-	64	247	164	295	297	279	-6.1%
Mazulia	000 M^2	-	-	37152	-	-	-	-	-	-
Tabaka za mbao	M^2	45147	44547	266	-	30589	35293	36935	38913	5.4%
Dawa za pareto	Tani	33	73	-	49	53	73	83	136	63.9%
Mbolea	Tani		-	25762	-	11200	0	-	-	-
Rangi	000 Lita	17451	24857	-	28201	31211	34868	36623	38308	4.6%
Bidhaa za petrol	000 Tani	-	-	1941	-	-	-	-	-	-
Saruji	000 Tani	1630	1756	34793	2313	2409	2581	2369819	2795687	18.0%
Chuma	Tani	52163	39969	34793	33384	39955	46690	48500	56752	17.0%
Bati	Tani	36492	31743	50664	71276	76912	81427	85314	86825	1.8%
Aluminium	Tani	110	105	58	59	33	23	37	27	-27.0%
Radio	000 namba	-	-		-	-	-	-	-	-
Betri	Milioni	75	53	78	93	89	68	75	93	24.0%

Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu na Wizara ya Viwanda na Biashara

Hakuna uzalishaji

Jedwali Na.4: Thamani ya Bidhaa Zilizouzwa Nje (Miln USD)

JUMUIYA/ NCHI	2005	2006	2007	2008	2009	2010	2011	2012p	2013r	2014p	2013/14 (Badiliko %)
JUMUIYA YA ULAYA NA USWISI	359.7	334.1	346.7	461.9	440.0	464.0	553.5	745.4	898.4	791.7	**-11.9%**
NCHI NYINGINE ZA ULAYA	259.9	421.6	454.2	533.3	469.0	687.1	828.5	816.8	16.9	77.5	**358.7%**
JUMLA - BARA LA ULAYA	**619.6**	**755.7**	**800.9**	**995.2**	**909.0**	**1151.1**	**1382.0**	**1562.2**	**915.3**	**869.2**	**-5.0%**
JUMUIYA YA NCHI ZA KUSINI MWA AFRIKA (SADC)											
Afrika ya kusini	275.4	268.9	176.1	232.5	170.9	416.8	831.1	967.9	760.5	689.1	**-9.4%**
Zambia	8.7	18.5	22.4	36.6	44.3	53.5	47.1	71.4	90.6	135.3	**49.4%**
Swaziland	0.6	1.9	0.2	0.6	20.8	0	12.5	2.2	4.1	1.2	**-71.9%**
Zimbabwe	1.6	1.2	0.7	1.2	5.7	0	4.1	4.7	6.5	7.1	**8.6%**
Msumbiji	6.5	10.6	19.1	31.4	20.3	17.7	61.9	53.1	66.4	68.1	**2.5%**
Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo	12.6	18.3	58.9	124	79.9	137.1	119.5	181.6	236.2	281.5	**19.2%**
Nchi nyingine za SADC	**16.9**	**21.7**	**23.7**	**17.1**	**32.3**	**0**	**82.6**	**141**	**44.9**	**53.7**	**19.6%**
JUMLA-SADC	**322.3**	**341.1**	**301.1**	**443.4**	**374.2**	**625.1**	**1158.8**	**1421.9**	**1209.2**	**1235.9**	**2.2%**
JUMUIYA YA AFRIKA MASHARIKI (EAC)											
Burundi	0	0	41.5	19.5	23.6	51.0	30.8	45.8	45.0	43.0	**-4.4%**
Kenya	76.3	97.2	101.1	235	177.4	297.3	211.2	330.9	227.1	445.9	**96.3%**
Rwanda	0	0	11.2	20.6	15.1	55.0	65.8	72.8	81.1	35.8	**-55.9%**
Uganda	20.1	20.5	19.3	40.5	47.7	46.8	44.6	65.8	66.1	73.3	**10.9%**
JUMLA – EAC	**96.4**	**117.7**	**173.1**	**315.6**	**263.8**	**450.1**	**352.4**	**515.3**	**419.3**	**598.1**	**42.6%**

JUMUIYA/ NCHI	2005	2006	2007	2008	2009	2010	2011	2012p	2013r	2014p	2013/14 (Badiliko %)
Nchi nyingine za Afrika	**34.7**	**29.9**	**72.8**	**96.1**	**0.6**	**5.8**	**67.9**	**47.7**	**3.5**	**340.9**	**9641.3%**
JUMLA – AFRIKA	**453.4**	**488.7**	**547.0**	**855.1**	**638.6**	**1081.0**	**1579.1**	**1984.9**	**1632.0**	**2174.9**	**33.3%**
BARA LA AMERIKA											
Marekani	16.5	20.7	34.2	55.1	39.5	46.5	47.5	66.8	60.5	143.0	**136.4%**
Canada	39.2	6	2.3	3.8	6.1	4.6	5.0	25.2	12.9	7.1	**-45.2%**
Nchi nyingine za Bara la Amerika	3.7	1.1	6	5.4	0	0	7.4	1.7	2.7	6.2	**127.9%**
JUMLA-BARA LA AMERIKA	**59.4**	**27.8**	**42.5**	**64.3**	**45.6**	**51.1**	**59.9**	**93.7**	**76.1**	**156.2**	**105.3%**
ASIA											
China	0	0	141.3	223.5	363.9	634.2	659.2	520.4	307.8	683.9	**122.2%**
India	63.2	63.8	77.3	171.8	183.8	218.5	202.7	476.5	748.2	1254.5	**67.7%**
Japan	68.7	82	57.1	136.9	164.7	209.7	346.8	296.5	220	247.8	**12.6%**
Umoja wa Falme za Kiarabu	33.7	47.3	88.4	65.4	66.8	55.3	74.9	93.2	84.2	85.5	**1.5%**
Hong Kong	9.6	7.6	14.1	13.4	85.6	12.6	11.1	23.1	30.4	35.6	**17.2%**
Singapore	18.7	4.4	4.0	11.0	6.4	13.5	10.9	24.3	55.7	15.9	**-71.4%**
Nchi nyingine za Asia	133.8	123.1	65.1	52.4	59.1	56.4	109.1	209.4	64.7	171.2	**164.6%**
JUMLA-ASIA	**327.7**	**328.2**	**447.3**	**674.4**	**930.3**	**1200.2**	**1414.7**	**1644.4**	**1511**	**2494.4**	**65.1%**
NCHI NYINGINEZO	**242.4**	**317.2**	**388.9**	**989.8**	**774.6**	**840.9**	**662.2**	**604.0**	**1214.5**	**65.5**	**-94.6%**

JUMUIYA/ NCHI	2005	2006	2007	2008	2009	2010	2011	2012p	2013r	2014p	2013/14 (Badiliko %)
JUMLA KUU	**1,702.50**	**1,917.60**	**2,226.60**	**3,578.8**	**3,298.1**	**4,324.3**	**5,097.9**	**5,889.2**	**5,348.9**	**5760.2**	**7.7%**

Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania na Wizara ya Fedha

p = Takwimu za Awali

Jedwali Na. 5 Wastani wa Bei za Mazao Makuu ya Chakula 2007/2008 hadi 2014/2015 (Mwenendo wa Bei ya Mazao ya Chakula Tsh/100Kg)

Mazao	2006/7	2007/8	2008/9	2009/10	2010/11	2011/12	2012/13	2013/14	2014/2015	%MABADILIKO(2013/14 - 2014/Machi, 2015)
Mahindi	18047	31727	37298	42133	34247	43308	65028	55854	38,133	-31.73
Maharage	57365	90670	107152	105092	109537	122868	131337	129957	137,957	6.16
Mchele	57779	90670	97213	99790	99721	152799	172654	132289	128,377	-2.96
Ngano	38056	69435	71342	79823	73694	75968	95196	101094	96,723	-4.32
Uwele	26441	41424	46033	47451	51512	75442	73085	84413	53,588	-36.52
Ulezi	35137	57806	61477	72593	71819	75442	105453	122607	106,600	-13.06
Mtama	23810	45673	46617	58270	51850	59878	70370	79894	54,446	-31.85

Chanzo: Wizara ya Viwanda na Biashara

Jedwali Na. 6: Thamani, Kiasi na Bei ya Bidhaa zilizouzwa Nje (2009-2014)

Bidhaa	2009	2010	2011	2012	2013	2014	2013/14 Badiliko (%)
Bidhaa Asilia:							
Kahawa	111.2	101.6	142.6	186.6	171.0	121.5	-29.0
Pamba	111.0	84.0	61.6	164.9	111.7	54.7	-51.0
Katani	6.7	10.9	16.9	18.4	16.9	16.8	-1.0
Chai	47.2	49.8	47.2	56.1	56.9	45.7	-19.7
Tumbaku	127.4	232.4	281.2	350.1	307.0	315.0	2.6
Korosho	68.6	96.9	107.0	142.6	162.4	222.2	36.8
Karafuu	14.4	7.6	28.9	38.1	43.0	52.9	23.2
Jumla	**486.4**	**583.2**	**685.5**	**956.7**	**868.9**	**828.8**	-4.6
Bidhaa zisizo asilia:							
Bidhaa za Petroli	0.0	0.0	0.0				
Madini	1274.8	1561.2	2283.4	2197.8	1782.1	1466.7	-17.7
Bidhaa za Viwanda	506.5	964.0	861.5	1037.3	1072.1	1239.6	15.6
Samaki na Mazao ya Samaki	155.0	150.4	137.7	160.6	130.6	195.0	49.4
Mazao ya Mboga na Maua	33.3	30.8	36.4	31.3	28.1	30.5	8.4
Bidhaa zilizouzwa tena	120.4	132.5	98.3	181.7	172.8	177.0	2.5
Bidhaa nyinginezo	282.9	338.2	330.2	555.7	517.6	687.2	32.8
Jumla	**2372.9**	**3177.0**	**3747.5**	**4164.4**	**3703.3**	**3796.1**	2.5
Bidhaa Zisizorekodiwa	438.9	564.0	664.9	768.2	685.8	693.7	1.2
JUMLA KUBWA	**3298.1**	**4324.3**	**5097.9**	**5889.2**	**5258.1**	**5318.7**	1.2

Chanzo: Idara ya Forodha, TRA

Jedwali Na. 7 Mwenendo wa Bei za Mifugo Tanzania (2010-2015)

Mnyama		2008	2009	2010	2011	2012	2013	2014	2015*	% Mabadiliko (2014 - 2015*)
Ng'ombe										
Majike	Daraja la II	313,747	331,077	343,402	384,422.66	424,683	426,071	430,694	465,824	8.20
	Daraja la III	235,781	249,433	249,550	307,652.41	338,833	320,180	334,418	356,101	6.48
Madume	Daraja la II	410,209	448,316	444,305	471,722.54	536,252	553,148	559,087	603,411	7.93
	Daraja la III	296,305	321,507	321,169	372,412.64	395,953	396,464	421,442	453,392	7.58
Madume +Majike	Daraja la II	706,514	769,822	765,473	844,135.17	932,205	949,611	980,528	1,056,803	15.51
Madume +Majike	Daraja la III	1,002,820	1,091,329	1,086,642	1,216,547.81	1,328,158	1,346,075	1,401,970	1,510,195	23.09
Mbuzi										
Majike	Daraja la II	34,560	39,853	40,455	45,626.25	49,907	50,801	54,986	59,546	8.29
	Daraja la III	27,159	29,098	29,860	34,584.94	35,872	35,332	38,820	45,273	16.62
Madume	Daraja la II	43,054	46,446	48,782	54,858.35	59,201	59,628	63,952	70,574	10.35
	Daraja la III	31,120	34,438	36,126	39,507.92	41,325	41,580	46,390	51,864	11.79
Madume +Majike	Daraja la II	74,174	80,884	84,909	94,366.27	100,526	101,208	110,342	122,438	22.14
Madume +Majike	Daraja la III	105,294	115,322	121,035	133,874.19	141,850	142,788	156,732	174,302	33.93

Mnyama		2008	2009	2010	2011	2012	2013	2014	2015*	% Mabadiliko (2014 - 2015*)
Kondoo										
Majike	Daraja la II	31,118	33,239	35,183	39,983.00	40,887	43,743	47,570	59,489	25.10
	Daraja la III	24,262	26,660	26,540	30,100.04	31,179	30,095	32,999	37,083	12.37
Madume	Daraja la II	36,654	39,883	43,955	47,766.44	48,486	51,150	58,359	72,142	23.62
	Daraja la III	27,033	30,924	31,656	34,520.52	33,378	34,864	38,394	43,273	12.71
Madume +Majike	Daraja la II	63,687	70,807	75,610	82,286.96	81,864	86,014	96,753	115,415	36.33
Madume +Majike	Daraja la III	90,720	101,731	107,266	116,807.48	115,242	120,877	135,148	158,688	49.04
Chanzo: Wizara ya Viwanda na Biashara										